# Nipashe

Jumanne Septemba 15, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580339

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Jaji Bomani amwagiwa sifa utumishi bora akiagwa Dar

UKURASA 2


Nipashe TESA

Jumanne Septemba 15, 2020

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Kijana anayetamani kusoma kozi awasaidie wengine

Kwa taarifa, ukame ni chanzo cha maradhi kama ilivyo mvua

Wanafunzi sasa waingia vitani kupigana mimba, ndoa utotoni

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

Mlipuko COVID-19 ulipotajwa kulipua mimba na ndoa utotoni

■Ndoa za wanafunzi ni usiku wa manane

■101 wapata ujauzito 'bye bye' shule

UKURASA 11

# Wanafunzi 10 wafa kwa moto shuleni

UKURASA 2



Mabaki ya bweni la wavulana katika Shule ya Msingi Byamungu Islamic, iliyoko Kata ya Itera wilayani Kyerwa, Mkoa wa Kagera, baada ya kuteketea kwa moto uliotokea usiku wa kuamkia jana na kusababisha vifo vya wanafunzi 10 na majeruhi sita. **PICHA: LILIAN LUGAKINGIRA**

## Wagombea wamwaga ahadi mpya

**NI** za JPM, Lissu, Seif, SAU na UMD...*Endelea*

*Ukurasa 3, 4 & 5*

## EU KUIPA TANZANIA BIL. 70/- ZA CORONA

UKURASA 4

**MICHEZO** ZLATKO: SIRI CARLINHOS KUPIKA BAO YANGA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

Fursa kwa Wagombea! 2020

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

VOTE

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiwa na marais wastaafu, Ali Hassan Mwinyi na Jakaya Kikwete, wakati alipowaongoza waombolezaji katika kuuaga mwili wa Mwanasheria Mkuu mstaafu, Jaji Mark Bomani kwenye viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam, jana. Wengine (kutoka kushoto) ni Jaji Mkuu mstaafu, Mohamed Chande Othman, Mawaziri Wakuu wastaafu, Cleopa Msuya na Joseph Warioba, Jaji mstaafu Damian Lubuva, Jaji Mkuu mstaafu Barnabas Samatta na (kulia) ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Adelardus Kilangi. **PICHA: OWM**

# Wanafunzi 10 Byamungu wateketea kwa moto

**Na Waandishi Wetu**

WANAFUNZI 10 wavulana wa Shule ya Msingi ya Kiislamu Byamungu, mkoani Kagera wameteketea kwa moto na wengine sita kujeruhiwa baada ya kuzuka moto huo ambao chanzo chake hakijajulikana.

Kufuatia tukio hilo, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, ameunda kamati ya watu sita kuchunguza chanzo chake, ikiwa ni tukio la tatu kutokea.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na vipimo vya vinasaba (DNA), vitatumika kutambua miili ya wanafunzi hao, kufuatia kuharibika.

Tukio hilo lililotokea usiku wa kuamkia jana, katika shule hiyo iliyoko kata ya Itera, wilayani Kyerwa mkoani Kagera, likiwa ni mfululizo wa matukio ya shule kama hizo kuungua pia katika maeneo tofauti nchini, ikiwamo jijini Dar es Salaam.

Julai mwaka huu, shule tatu za Mivumoni Islamic Seminari na Kinondoni ziliteketea kwa moto na wanafunzi wawili kufariki.

Shule ya Mivumoni Islamic Seminari iliyopo msikiti wa Mtambani Kinondoni, ikiteketea kwa moto mara tatu mwaka huu, kwa kipindi cha miezi miwili.

Mufti Mkuu wa Tanzania, Aboubakar Zuberi, alipotafutwa kwa njia ya simu na Nipashe kuzungumzia suala hilo, alisema atatolea ufafanuzi, lakini alipotafutwa tena muda alioahidi simu yake haikupokelewa.

**RC KAGERA**

Akizungumza katika eneo la tukio jana, Brigedia Jenerali Gaguti, alisema ameifunga kwa muda wa wiki moja, Shule ya Byamungu na kuvitaka vyombo vya ulinzi na usalama kuanzia ngazi za vijiji hadi mkoa, kufanya mapitio upya ya shule zote za bweni katika mkoa huo, kuhakikisha kama zina vibali halali vya kuruhusu malazi katika mabweni.

"Kamati hii inapaswa kuhakiki ubora wa majengo, mifumo ya umeme na mifumo ya milango na madirisha kama yanaruhusu watoto kujiokoa linapotokea tukio la moto," alisema.

Alisema kwamba ikibainika baadhi ya shule hazina vigezo hivyo, hatua za haraka za kuzifungia zichukuliwe.

"Viongozi wa Shule ya Msingi ya Byamungu Islamic watakuwa chini ya uangalizi wa kamati ya ulinzi na usalama, ili kutoa ushirikiano kuhusiana na tukio hilo."

"Kwa sababu shule hii haina darasa la saba wanaotarajiwa kufanya mtihani wa taifa hivi karibuni, naifunga kwa muda wa wiki moja, ili kuruhusu wanafunzi kupata faraja na kurejea katika hali yao ya kawaida," alisema Brigedia Jenerali Gaguti.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, Revocatus Malimi, alisema kuwa kutokana na miili ya wanafunzi hao kuharibika, imekuwa vigumu kuitambua na kwamba zinafanyika taratibu za utambuzi wa kitaalamu.

"Vitafanyika vipimo vya vinasaba (DNA) kwa wazazi wote ambao watoto wao hawaonekani, ili kuwatambua na hii ni kutokana na miili yao kuharibika vibaya," alisema mkuu huyo wa mkoa.

Alisema hadi sasa hakuna taarifa zozote kuhusu chanzo cha tukio hilo na uchunguzi unaendelea.

**ZIMAMOTO**

Mkuu wa Jeshi la Zimamoto Mkoa wa Kagera, Hamis Dawa, alisema wilaya hiyo haina ofisi za zimamoto na kuwa inahudumiwa na Wilaya ya Karagwe na kwamba askari wake walijitahidi kuwahi eneo la tukio ili kutoa msaada.

HOSPITALI

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Nyakahanga iliyoko wilayani Karagwe, Dk. Furaha Kahindo, alisema wamepokea miili 10 ya wanafunzi hao na majeruhi sita na kuwa wawili kati yao hali zao ni mbaya.

"Kwa majeruhi wanne tuna uwezo wa kumudu matibabu yao na hali zao zinaendelea kuimarika taratibu, lakini majeruhi wawili hatuwezi kuwamudu tunafanya utaratibu wa kuwapatia rufani kwenda katika hospitali kubwa hasa ya kanda ambayo ni Bugando iliyoko Mkoa wa Mwanza," alisema.

**MKUU WA SHULE ASIMULIA**

Naye Mkuu wa shule hiyo, Suleiman Abdul, alisema moto huo umeteketeza bweni la wavulana lililokuwa na wanafunzi 74, na kuwa taarifa za moto zilitolewa na mlezi wao anayelala nao bwenini, ambaye amewezesha kupatikana kwa msaada wa kuuzima kutoka kwa wananchi.

Abdul alikiri kupoteza watoto 10 na kupata majeruhi sita, katika shule hiyo yenye jumla ya wanafunzi 127 wa kike na kiume, kuanzia darasa la kwanza hadi la sita.

**DC: TUSILAUMIANE**

Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa, Rashid Mwaimu, lilikotokea tukio hilo, alisema kwa sasa hawawezi kumlaumu mtu yeyote na kwamba vyombo vya ulinzi na usalama vitafanya uchunguzi na kubaini chanzo cha tukio hilo.

"Kwa sasa hatuwezi kumlaumu mtu yeyote, tuwe na subira, lakini niwape pole wazazi wote ambao watoto wao wamepoteza maisha katika tukio hili, Mwenyezi Mungu awape uvumilivu," alisema Mwaimu.

Aliwashukuru wananchi wa Kyerwa hasa wanaoishi jirani na shule hiyo kwa kujitokeza kuzima moto na kuokoa watoto waliokuwa katika jengo lililoungua na kuwataka kuendelea na ushirikiano huo.

MATUKIO YA MOTO

Kwa kipindi cha miezi miwili, linakuwa tukio la tatu katika shule hiyo. Tukio la kwanza lilitokea Julai 18, moto wa muundo huo na ulizimwa, Julai 23, tukio lingine lilitokea likiwa nila tatu mfululizo ndani ya eneo moja.

"...Ni matukio ambayo yanaendelea kutokea ndani ya hizi shule za Kiislamu za jijini Dar es Salaam, uchunguzi umefanyika na msemaji wa hili ili kujua chanzo ni nini ataitoa Mkuu wa mkoa," alisema Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Zimamoto.

LISSU ATOA POLE

Mgombea wa urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu jana alituma salamu za rambirambi kwa familia zilizopoteza ndugu zao katika tukio la moto mkoani Kagera na kuvitaka vyombo vinavyohusika kufanya uchuguzi wa haraka kubaini chanzo cha tukio hilo.

Akihutubia wananchi katika mkutano wa kampeni mjini Mafinga, mkoani Iringa alisema, "kuna vitu vingine vinahitaji kuchunguzwa ili kupata majibu sahihi kama ni uzembe au ni mipango ya Mungu. Inawezekana siyo amri ya Mungu bali ni mkono wa binadamu, ni vyema vyombo vinavyohusika kufanya uchunguzi wa jambo hili haraka," alisema Lissu.

Julai mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, akizungumza katika Baraza la Eid, Viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam, alisema ameunda tume kuchunguza matukio ya moto jijini humo na alimwagiza Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, kuunda kamati ya uchunguzi.

# Waziri Mkuu aongoza mamia kumuaga Bomani

**Na Beatrice Moses, TUDARCO**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, jana ameongoza mamia na wananchi kuaga mwili wa Hayati Mwanasheria Mkuu wa kwanza mzalendo, Mark Bomani, aliyefariki dunia Septemba 10, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Hafla ya kuaga mwili wa Jaji Bomani ambaye alikuwa ni miongoni mwa wajumbe wa Bodi ya Wadhamini wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), ilifanyika katika viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika tukio hilo, Majaliwa alisema Bomani alikuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa kwanza mzalendo, alisaidiana na Mwanasheria Mkuu wa kipindi hicho, Roland Brown katika kutayarisha nyaraka zote za kisheria za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

"Kati ya mwaka 1965 hadi 1976, aliteuliwa kushika nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa kwanza mzalendo, nafasi ambayo alitumikia taifa kwa uaminifu, uadilifu na umahiri mkubwa," alisema Majaliwa.

"Bomani alikuwa ni mmoja wa wajumbe wa Bodi ya Udhamini ya CCM hadi umauti ulipomkuta, ambapo kwa kushirikiana na wenzake wamemudu kusimamia kwa uadilifu mkubwa mali za chama hicho."

Waziri Mkuu kwa niaba ya Rais John Magufuli, alitoa pole kwa familia, wananchi kwa kuondokewa na Bomani ambaye ni miongoni mwa watu wenye historia ya kipekee kwa Tanzania.

"Watanzania wote tutamkumbuka kwa kazi kubwa aliyoifanya katika kamati mbalimbali kupitia sheria na kuleta mabadiliko, Bomani alikuwa ni Mjumbe wa Tume ya Rais iliyoundwa kutoa mapendekezo ya mfumo mpya wa demokrasia wa chama kimoja," alisema Majaliwa.

Pia alikuwa Mwenyekiti wa Tume ya Utangazaji, Mwenyekiti wa Kamati kupitia Sera ya Madini ambaye iliwezesha kutungwa kwa sheria ya madini, mshauri wa kisheria wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Pia alisema Bomani enzi za uhai wake amewahi kuwa mshauri wa masuala ya kisheria na Katiba katika nchi ya Namibia baada ya kupata uhuru, pamoja na kuwa mshauri wa chama cha FRELIMO katika kuandaa Katiba mpya ya Msumbiji.

"Natoa pole kwa wanataaluma ya sheria kwa kuondokewa na mtu muhimu katika tasnia hiyo, ambaye alitoa mchango mkubwa kwa kupitia taaluma hiyo katika nafasi mbalimbali alizotumikia akiwa ndani na nje ya nchi," alisema.

Mwili wa Bomani ulitolewa katika viwanja hivyo vya Karimjee na kupelekwa kwenye Kanisa la Waadventista wa Sabato, Mwenge alikokuwa akiumini, iliandaliwa ibada ya faraja ya msiba.

Akihubiri katika ibada hiyo Askofu Mkuu wa Jimbo la Mashariki Kati mwa Tanzania wa Kanisa la Waadvenista wa Sabato, Joseph Mngwabi, aliwataka watu kufanya kazi kwa bidii kulingana na karama walizojaliwa na Mungu.

"Mauti ni ya ovyo inachukuwa watu muhimu, kama Mungu amekupa kipaji kitumie kwa uaminifu uache alama," alisema Askofu Mngwabi.

Mchungaji Petro Mganda wa Kanisa hilo Mwenge aliongoza ibada hiyo chini ya neno kutoka Ufunuo 14:13 lisemalo: "Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, andika heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao; kwa kuwa matendo yao yafuatana nao."

Baada ya ibada hiyo mwili wa Bomani ulipelekwa kwa ajili ya maziko.

**HABARI KITAIFA**

# JPM kujenga uchumi bila kutegemea wafadhili



**Na Gwamaka Alipipi, CHATO**

MGOMBEA urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amesema dhamira yake ni kujenga nchi katika uchumi wa kujitegemea, kwa kutekeleza miradi ya mikubwa ya kimaendeleo kwa fedha za ndani pasipo kutegemea wafadhili.

Alitoa kauli hiyo jana mkoani Geita wilayani Chato, wakati akiwahutubia maelfu ya wananchi na wanachama wa CCM katika Uwanja wa Mazaina kumsikiliza akiomba kura, pamoja na kueleza mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano.

"Wapo watu wana mawazo ya kupata fedha kutoka kwa wafadhili, hivi hao wafadhili wao hawataki kuishi huko kwao? Yaani wafadhili wakuletee wewe. Ukichukua fedha za wafadhili lazima utarejesha mara mbili, ndiyo maana tukaamua kutekeleza miradi yetu kwa fedha zetu, tunataka kuijenga Tanzania yenye uchumi wa kujitegemea," alisema Dk. Magufuli na kuongeza:

"Nimekaa Wizara ya Ujenzi, Ardhi, pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, najua ukitegemea cha ndugu hufa maskini, maana yake wanataka kutunyonya, tunataka kujitegemea wenyewe."

Alisema katika kipindi cha miaka mitano mambo mengi yamefanyika nchini ikiwamo ujenzi wa barabara, madaraja makubwa likiwamo la Busisi-Kigongo, ujenzi wa reli ya kisasa, Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano nchi imekutana na changamoto nyingi za kiuchumi, kiusalama, lakini serikali ilishikamana na kufanikiwa kuleta mafanikio.

Alisema: "Wakati naingia madarakani nchi yetu ilikuwa ya uchumi wa kimaskini, leo inatambulika ni ya uchumi wa kati, baada ya kuingia madarakani tumejenga zahanati 1,200 nchi nzima, vituo vya afya 487, hospitali 98 za wilaya, hospitali za mikoa 10, hospitali za rufani tatu na zingine zinakuja, haya yote ni mafanikio, lakini bajeti ya dawa imeongezeka kutoka Sh. bilioni 31 hadi Sh. bilioni 270."

Alisema kwa kipindi cha miaka mitano serikali iliamua kujikita katika fedha zinazopatikana kuwekeza katika kuboresha sekta ya afya, ujenzi wa miundombinu, sekta ya elimu na ujenzi wa miundombinu.

"Katika miundombinu nyie ni mashahidi, kwenye vivuko Ziwa Victoria watu walikuwa wanakufa kwa sababu walikuwa wanatumia mitumbwi, tulipoingia madaraka tukasema haiwezekani tukaamua kutenga Sh. bilioni 152 kukarabati meli zote na kununua meli kubwa yenye uwezo wa kubeba watu 1,200 na tani 400 za mizigo. Lengo ni kuwakomboa wananchi kwenye usafiri," alisema.

Dk. Magufuli alisema ameamua kujitoa maisha yake ya kiuongozi kama sadaka kwa Watanzania, kwa kufanya mambo ya kimaendeleo kwa kuwajali maskini.

UJENZI WA VIWANDA

Kuhusu viwanda, Dk. Magufuli alisema serikali imejenga viwanda vipya 8,440 katika kipindi cha miaka mitano ambavyo vimetengeneza ajira nyingi. Alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha inarudisha viwanda vilivyoachwa na hayati Mwalimu Julius Nyerere.

UHUSIANO KIMATAIFA

Dk. Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano Tanzania imeweza kufungua balozi katika nchi nane.

**ULINZI NA USALAMA**

Dk. Magufuli alisema katika kipindi cha miaka mitano serikali imefanikiwa kudumisha amani na usalama nchini.

Alisema wakati anaingia madarakani, wilayani Kibiti mkoani Pwani kulikuwa na mauaji, askari 12 waliuawa kwa kupigwa risasi, lakini serikali iliweza kusimamia na kurudisha amani.

Aliongeza kuwa endapo Tanzania ikikosa ulinzi na usalama hakuna shughuli yoyote itakayofanyika, kwamba aliwaonya Watanzania kutokulewa na uhuru uliopo sasa kwani endapo ikitoweka majuto yake ni makubwa.

# Mgombea UMD kufuta Vitambulisho vya Taifa

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama cha Union for Multiparty Democracy (UMD), Mohamed Mazrui, amesema iwapo atapata ridhaa ya kuongoza Tanzania, serikali yake itafuta utaratibu wa wananchi kupewa Vitambulisho vya Taifa.

Alisema hayo juzi wakati wa mkutano wa kampeni uliofanyika Mbagala, jijini Dar es Salaam.

Mazrui alisema, baada ya kufuta utaratibu wa kutoa Vitambulisho vya Taifa, wananchi watapewa hati za kusafiria (passport) ambazo zitatolewa bure nchi nzima.

Alisema, hati hizo zitawawezesha wananchi hao kusafiri katika nchi yoyote kwa ajili ya kwenda kutafuta maisha, bila vikwazo vyovyote.

Kuhusu ajira, alisema serikali yake itapunguza masharti kwa wawekezaji, ili waweze kuwekeza kwa wingi na hivyo kuongeza ajira kwa wananchi.

Mazrui alisema, wakulima watanufaika kwa kutafutiwa wanunuzi wa kimataifa ambao watanunua mazao kwa bei nzuri.

"Wakulima tutawaondolea suala la stakabadhi ghalani badala yake tutawaletea wanunuzi wa mazao kutoka nje," alisema.

Aliongeza kuwa, serikali yake itaondoa utaratibu wa kulipa kodi ya majengo, ambayo imekuwa kero kwa wananchi.

Vilevile, alisema hivi sasa wananchi wanatozwa kodi ya majengo, lakini katika hali ya kushangaza huduma kama za taka wanatozwa tena fedha jambo ambalo linaleta usumbufu.

Alisema, walimu wataongezewa mishahara na elimu itaboreshwa na kuwa bure japo wananchi watachangia kiasi kidogo.


**BAM INTERNATIONAL BV TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**MNADA WA HADHARA:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na **BAM International Tanzania.** watauza kwa mnada wa hadhara Makontena matupu, Mitambo ya ujenzi na vifaa vya ujenzi tarehe 19 Septermbe , 2020 siku za Jumamosi saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika BAM International eneo la mradi Batching Plant (Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere) Terminal 3 Dar es salaam.

**VIFAA VYA UJENZI NA FANICHA ZA OFISI ZITAKAZOUZWA:**
Mobile Fencing, Manhole covers, Aluminum Profile, Galvanized street light poles, Steel and aluminum Scaffoldings, Podium Ladder, Pipe hard insulations, Mesh, Electrical items, Welding rods, Knauf Insulation materials, Sandwich panels, Fire Fighting fittings, Hose & Valves, Ceiling Tiles, Floor Tiles, Canon Photo Copy m/c C5235, Plotter HP 520,File Cabinets, Office Table, Chairs, Construction Plastic Spacers, Armoured Cables, Vyuma Chakavu na vingine vingi.

**MAKONTENA NA MITAMBO YA UJENZI YATAKAYOUZWA KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI**

| Idadi | Aina | Model | Hali yake | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 47 | Empty Container 40FT. | High Cub, STD& Open Top | Nzuri | Bado |
| 8 | Pipe welding/Threading m/c | 160mm | Nzuri | Bado |
| 4 | Welding m/c 250/ Invater | 250 / 522 / 3- phase | Nzuri | Bado |
| 2 | Table Saw machine | ZBV -450 | Nzuri | Bado |
| 4 | Floor cutting machine | Honda | Nzuri | Bado |
| 5 | Converter Poker Vibrator | LAIE 2 | Nzuri | Bado |
| 3 | Multi stage pump | 11Kw / 15 - HP | Nzuri | Bado |
| 4 | Terrazzo Grinding machine | 3 phase | Nzuri | Bado |
| 12 | Assorted Terrazzo Machine | Vacuum cleaner/ Polish | Nzuri | Bado |

Mali zote zitakaguliwa BAM International eneo la mradi Batching Plant JNIA T3 Dar es Salaam, Tarehe 16 mpaka 18 September, 2020 kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 10:00 jioni

**MASHARTI YA MNADA:**

1. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 5 za kazi kabla ya Sept.25,020 saa 10:00 jioni kwenye bank Akaunti ya BAM utakayoelekezwa, ukishindwa kulipa kwa muda huo mali itauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
3. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
4. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi .
5. Kila mtu atatakiwa kuwa na bid namba itakayo patikana getini,

**Kwa maelezo zaidi waone:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO. 5 "E" LION STREET SINZA**
**DAR ES SALAAM**
**CELL NO: 0754 284 926,**
**E-mail: universalauction@hotmail.com**

215900102


# Mgombea wa SAU ataja serikali mseto

**Na Sabato Kasika**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama cha Sauti ya Umma (SAU), Muttamwega Mugaywa, amesema akishinda uchaguzi mkuu, ataunda serikali ya mseto ili kila Mtanzania achangie maendeleo ya nchi yake bila kujali chama.

Alisema hayo wakati akihutubia kwenye uzinduzi rasmi wa kampeni zake uliokwenda sambamba na uzinduzi wa ilani ya chama hicho katika Jimbo la Ukonga, jijini Dar es Salaam juzi.

Katika uzinduzi huo, mgombea huyo alihutubia katika viwanja vya Kwa Zoo vilivyopo Chanika kisha Ukonga Mombasa, na kusisitiza umuhimu wa kuwa na serikali za mseto.

"Serikali yetu itafanya utaratibu wa kubadilisha katiba, ili kuunda baraza la mawaziri mchanganyiko, kwani ni muhimu tushirikiane, ili kila mmoja achangie maendeleo ya nchi yake," alisema Mgaywa.

Alisema, anatamani kupata waziri mkuu kama Kassim Majaliwa, kwa madai kwamba ni mchapakazi, ambaye amekuwa mfano mzuri kwenye serikali ya awamu ya tano kwa kufuatilia maelezo ya Rais John Magufuli.

Alisema, Watanzania wanataka maendeleo, na kwamba maendeleo hayana chama, hivyo ni muhimu kuwa na serikali ya mseto, bila kujali chama kwa vile kila Mtanzania ana mchango kwa maendeleo ya nchi yake.

"Serikali ya CCM imefanya makubwa sana, lakini siyo vibaya ikatupisha na sisi SAU tuendeleze pale ambapo imeishia na tutaunda serikali ya mseto, ambayo watu kutoka vyama mbalimbali hata wa CCM," alisema.

Mbali na hilo, alisema, akiwa rais atahakikisha serikali ya chama chake inakuwa na wizara 12 tu, ambazo amedai zinatoshwa, na kwamba haoni sababu yoyote ya kuwa na utitiri wa wizara.

"Vile vile chini ya serikali ya SAU, hakutakuwa na bodi ya mikopo, bali bodi ya kusomesha kila mtu, ili Watanzania wote wapate elimu ya juu kuliko hivi sasa ambapo mikopo imekuwa na changamoto nyingi," alisema.

Aliongeza kuwa, kipindi ambacho serikali yake itakaa madarakani, itanunua ndege 30, itatoa ajira milioni tisa kila mwaka, huku kima cha chini cha mshahara kikiwa Sh. milioni moja na sekta binafsi Sh. 500,000.

"Lakini pia SAU tuna vipaumbele vyetu ambavyo ni afya, elimu na kilimo na viwanda, tunataka wajawazito wapate huduma ya afya bure bila usumbufu wa kwenda na ndoo na vifaa vingine vya kujifungulia," alisema.

Kwa upande wa kilimo, alisema, sekta hiyo ndiyo yenye changamoto nyingi ambazo zinasababisha wakulima nchini wasinufaike, kwa madai kwamba wengi wao wanatumia jembe la mkono.

"Tukiingia madarakani tutahakikisha wakulima nchini wanatumia trekta, ili wanufaike na kilimo huku mazao yao yakiuzwa kwa bei nzuri kuliko ilivyo sasa na pia wafanyabiashara wadogo wakiwamo mama lishe, baba lishe, kila mmoja atapewa shilingi milioni moja aboreshe biashara zake," alisema.

Aidha, alisema amejitosa kuwania nafasi hiyo, kwa kuwa ana sifa tatu muhimu zinazotakiwa ambazo alizitaja ni uzalendo, uadilifu na uwajibikaji na kuwaomba wananchi wampe kura awe rais.

HABARI KITAIFA

# EU kuipa Tanzania bil. 70/- kuikabili corona

**Na Mwandishi Wetu**

UMOJA wa Ulaya (EU), umesema uko tayari kutoa Sh. bilioni 70 kwa Serikali ya Tanzania kwa ajili ya kusaidia mipango ya kukabiliana na janga la corona na madhara yake kiuchumi.

Hayo yalisemwa na Rais wa Baraza la Umoja wa Ulaya, Charles Michel, wakati akipokea hati za utambulisho za Balozi wa Tanzania nchini Ubelgiji, ambaye ni Mwakilishi wa Tanzania katika Umoja wa Ulaya, Balozi Jestas Abuok Nyamanga.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, hafla hiyo ilifanyika jana katika Makao Makuu ya Umoja huo, Brussels, Ubelgiji.

Rais Michel alisema, sehemu ya fedha hizo zinalenga kutumika kuweka miundombinu ya umeme na maji katika hospitali, vituo vya afya na zahanati zilizojengwa na serikali.

Alisema hiyo ni hatua ya EU kuunga mkono juhudi hizo muhimu zilizofanywa na serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli katika kupambana na virusi vya corona na taratibu za kutoa fedha hizo ziko katika hatua za mwisho.

"Umoja wa Ulaya uko tayari kuendelea kuongeza wigo wake wa ushirikiano na Tanzania na nchi zingine za Afrika katika kukabiliana na janga la corona na madhara yake kiuchumi," alisema.

Kwa upande wake, Balozi Nyamanga alieleza umuhimu wa Umoja wa Ulaya kuondoa marufuku za safari kwa nchi, ambazo maambukizi ya corona yamedhibitiwa ikiwamo Tanzania.

Alisema hali hiyo itawezesha kukua kwa sekta za utalii na sekta zingine za uchumi wa nchi hizo.



Mgombea urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akihutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika kijiji cha Ikanga, Kata ya Mdabulo, Jimbo la Mufindi Kaskazini, mkoani Iringa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lissu aahidi neema wakulima chai, mbao

**Na Elizabeth Zaya**

MGOMBEA wa urais wa Jamhuri ya Muungano kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema kutokana na utajiri mkubwa uliopo katika mkoa wa Iringa unaotokana na mbao na chai, ulitakiwa uwe kitovu cha viwanda vya kutengeneza samani katika nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Alisema akichagulia kuwa rais, atahakikisha anabadilisha utajiri wa rasilimali zilizopo katika mkoa huo za mbao na chai kunyanyua uchumi wa mkoa huo.

Lissu alitoa kauli hiyo wakati akihutubia katika kampeni katika maeneo ya Mufindi Kaskazini na Mafinga mkoani humo.

Alisema pamoja na utajiri uliopo katika mkoa huo unaotokana na rasilimali zake, lakini wananchi wake wameendelea kubaki maskini.

Lissu alisema akichaguliwa kuwa Rais, atahakikisha kwamba anatumia rasilimali zilizopo katika mkoa huo kuinua uchumi katika mkoa huo na kumaliza changamoto zote zilizopo kwa sasa.

Alisema serikali ya chama hicho itabadili mfumo wa utawala ili mali za wananchi katika kila eneo zimilikiwe na wananchi wenyewe na siyo kutoka mbali.

Pia alisema ataondoa kodi zote ambazo wakulima wa miti na chai wamekuwa wakitozwa ili wanufaike na kilimo cha mazao yao katika kuwaletea maendeleo.

Alisema mkoa huo mpaka sasa bado umeendelea kukumbwa na changamoto mbalimbali ikiwamo kukosa barabara za rami na pamoja na kuwa na mali nyingi.

"CHADEMA tunasema hivi, mkituchagua tutatengeneza utaratibu wa kusimamia rasilimali za kilimo cha miti na mazao ya mbao na chai katika Mkoa wa Iringa, wilaya inayoongoza kwa utajiri katika nchi hii ni Mufindi na nchi hii imejengwa kutokana na mbao zinazotoka katika wilaya hii, lakini bado wananchi wake ni masikini," alisema Lissu.

"Sisi CHADEMA lazime tushughulikie changamoto zote hizi endapo tutachaguliwa kuingia madarakani, tunataka wananchi wanufaike na rasilimali zao na siyo watu wengine kutoka mbali."

"Na ndiyo maana tunasisitiza kwamba lazima tuwe na Katiba mpya ambayo itaeleza kwa uwazi kwamba wananchi ndio wenye mamlaka na mali zao."

# CCM, CHADEMA vyalia mabango yao kuchanwa

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Shinyanga, kimelaani tabia ya baadhi ya vijana wanaodhaniwa kuwa ni wa upinzani kuchana mabango ya mgombea urais wa chama hicho, Dk. John Magufuli.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, alitoa malalamiko hayo jana wakati akizindua kampeni za CCM Jimbo la Shinyanga Mjini, zilizofanyika kwenye Kata ya Ngokolo, mjini humo.

Alisema tabia iliyoanza kufanywa na vijana wa upinzani kuchana mabango ya mgombea wao wa urais, Dk. John Magufuli, haitavumilika na atakayekamatwa atachukuliwa hatua kali.

"Naombeni vyama vya upinzani tufanyeni kampeni za kistaarabu ili uchaguzi uishe kwa amani sasa hivi kuna vijana wenu wameanza kuchana mabango ya mgombea wetu wa urais pamoja na kuyaandika maneno machafu hili siyo sawa," alisema Mlolwa. Naye Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Gasper Kileo, alisema uchunguzi walio ufanya umebaini kuwa vijana wanaochana mabango hayo wanatoka Musoma na wamepanga kuchana mabango yote yaliyopo barabara kuu.

Kwa upande wake, mgombea ubunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini (CCM), Patrobas Katambi, alikemea kampeni za kuchafuana kwenye majukwaa na kuwataka wagombea wenzake washindane kwa hoja kuhusu nini wanatarajia kuwafanyia wananchi iwapo watachaguliwa. Alisema endapo watamchagua kuwa mbunge wao Oktoba 28, mwaka huu, ataboresha sekta ya afya, elimu, mifugo, kilimo, uwekezaji wa viwanda, kutoa mikopo kwa vijana na wanawake na kuweka miundombinu ya mzunguko wa kifedha.

Wakati huo huo, Francis Godwin, kutoka Iringa anaripoti kuwa kasi ya uchanaji wa mabango ya wagombea wa vyama vya CCM na CHADEMA imeongezeka katika Jimbo la Iringa Mjini, huku uongozi wa vyama hivyo ukilaani vitendo hivyo.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Katibu wa CCM Mkoa wa Iringa, Brown Mwangomale, alisema imezuka tabia ya baadhi ya watu wanaosadikika kuwa ni wafuasi wa CHADEMA kuzunguka usiku mitaani na kuchana mabango ya mgombea urais wa CCM, Dk. John Magufuli.

Alisema vitendo hivyo si vya kiungwana na kwamba wakimkamata mtu ama watu wanaotekeleza vitendo hivyo hawatasita kuchukua hatua dhidi yao.

Katibu huyo alisema tayari wameanza kufanya msako mitaani na kuchukua hatua dhidi ya vijana wanaotumika kuchana picha za mgombea urais wa CCM na wagombea wengine kwa kuwafikisha kituo cha polisi. Mwangomale alisema hawazuii chama chochote kuweka mabango katika maeneo ambayo CCM imeweka mabango ya wagombea wake, lakini hawatakubali kuona mabango ya wagombea wao yakichanwa ama kuondolewa na kuwekwa mabango ya wagombea wa vyama vya upinzani.

Mwangomale alisema tayari wamemkamata kijana mmoja ambaye alikutwa akichana bango la mgombea urais wa CCM na kumfikisha polisi. Mgombea ubunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa (CHADEMA), alisema hadi sasa mabango yake yamefanyiwa hujuma kubwa na watu wanaodhaniwa kuwa ni wafuasi wa CCM kupaka rangi mabango yake yote.

Msigwa alitoa malalamiko hayo juzi katika mkutano wake wa uzinduzi wa kampeni uliounganishwa na mkutano wa kampeni za mgombea urais wa CHADEMA, Tundu Lissu.

# Maalim Seif kuigeuza Z'bar kituo cha biashara

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT -Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amepokewa kwa kishindo kisiwani Pemba na kuwahutubia maelfu ya wananchi na wafuasi wa chama hicho katika mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya Tibirinzi na kuahidi kuigeuza Zanzibar kuwa kituo cha biashara.

"Bado CCM ambao wametawala kwa miaka zaidi ya 50, hawajaitendea haki Zanzibar na kuwafanya vijana walio wengi kukosa ajira," alisema.

Aliwataka wananchi kutoziharibu kura zao kwa kuvipigia kura vyama vingine.

"ACT inasikitishwa sana na umaskini uliopo Zanzibar, na nikishaingia madarakani hilo litakuwa historia hapa Zanzibar kwa sababu nitaigeuza kuwa kituo cha biashara," alisema.

Katika hatua nyingine, Maalim Seif alisema Zanzibar itaongozwa kisheria na kila mmoja kupata haki yake, bila kujali unyonge wa mtu.

"Mwaka 2015, mlikuwa mashuhuda, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, mliona ilivyopindwa, lakini serikali ijayo chini ya Maalim Seif sheria itafuatwa," alisema.

Pia alisema hakuna mwananchi yeyote atakayenyimwa haki yake, ikiwamo kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi.

"Hivi sasa wapo watu kutoka nje ya Zanzibar wamekuwa wakipewa vitambulisho hivyo na kuwakosesha wale wenye haki hiyo," alisema.

Alisema serikali yake itatoa haki ya uhuru wa vyombo vya habari ili kufanyakazi zake bila ya bughudha.

"Lazima vyama vifanye mikutano ili kueleza makosa ambayo tunayo ili na sisi tuyachukulie hatua ya kuitatua."

Aliahidi kuitumia serikali yake kuondoa ukabila na ubaguzi na kwamba ataleta umoja wa kitaifa kwa Wazanzibar wote.

"Pemba tunakusudia kujenga bandari moja kubwa ambayo itaweza kupokea meli kubwa za makontena ili karafuu zisafirishwe moja kwa moja hadi soko la dunia," alisema.

Kuhusu bei za vyakula Pemba, alisema zimekuwa ghali mno kwa sababu hakuna bandari kama hiyo na kueleza katika miaka yake mitano vyakula vitashuka bei kama ilivyo kisiwani Unguja.

Kuhusu ajira aliahidi katika uongozi wake wa miaka mitano ya kwanza vijana wote watakuwa na ajira.

Ngome ya wanawake ya chama hicho Zanzibar imeuahidi mgombea huyo ushindi mkubwa katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28.

Mwenyekiti wa ngome hiyo, Halima Ali, alisema wanawake kisiwani Pemba wamejipanga kuhakikisha kuwa mgombea wao anashinda kwa ushindi mkubwa.

"Maalim Seif sisi tumeshamaliza kazi na kama kampeni si sheria sisi tungalikuambia usifanye kampeni, lakini sisi tumemaliza kazi ya kukupa wewe ushindi mkubwa," alisema Halima.



Mgombea mwenza wa kiti cha urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na wanachama wa chama hicho na wananchi wa kijiji cha Mchomoro, alipokuwa njiani akielekea Namtumbo mjini kwa ajili ya kuhutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu, jana. **PICHA: OMR**

# CHADEMA yaitaka NEC kuwapa barua waliorejeshwa

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, ameitaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kuwapatia barua wagombea wake wote ambao rufani na mapingamizi yao yameshashughulikiwa.

Pia Mnyika alisema ameiandikia tume hiyo kuitaka iwarejeshe wagombea wake wote waliokuwa wameenguliwa ili waanze kufanya kampeni.

"Haiwezekani mpaka sasa tume iwe haijamaliza kushughulikia rufani na mapingamizi, tunaitaka itoe barua na iwarejeshe wagombea wetu wote," alisema Mnyika.

"Inasikitisha kwamba mpaka sasa (jana) ikiwa ni siku ya 18 ya kampeni bado wagombea wetu ambao walienguliwa rufani zao hazijashughulikiwa, sehemu kubwa ya rufani wagombea wetu wana nafasi ya kurejeshwa, tunaomba warejeshwe."

Akijibu hoja hiyo, Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, alisema tume bado inashughulikia rufani zote na mpaka kesho itakuwa imemaliza kushughulikia rufani na mapingamizi yote.

"Bado rufani zinashughulikiwa na tunafanya kazi hadi usiku wa manane, na tunaamini kufikia Jumatano (kesho), kazi yote itakuwa imemalizika," alisema Dk. Mahera.

Akijibu hoja kuhusu barua za rufani na mapingamizi inayoshughulikia, Dk. Mahera alisema wagombea ambao wameshinda rufani zao, barua zao zote zinapatikana katika ofisi zilizopo katika maeneo yao.

"Ni kweli tumepokea barua kutoka CHADEMA, barua zote za rufani na mapingamizi tunazoshughulikia za wanaofanikiwa kushinda na wasioshinda, zote zinapatikana katika maeneo yao waliko wagombea, waende huko watapata barua zao na tumejitahidi kufanya kazi hii hadi usiku wa manane," alisema Dk. Mahera.

# 24 warejeshwa udiwani

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imekubali rufani 24 na kuwarejesha wagombea udiwani katika orodha ya wagombea.

Taarifa iliyotolewa jana jioni na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa (NEC), Dk. Wilson Mahera, ilizitaja rufani hizo kuwa ni kutoka kwenye Kata za Mlangarini (Arumeru Mashariki), Nduruma (Arumeru Magharibi), Nkunguru (Magu), Ibungilo (Ilemela) na Itumbili (Magu).

Ilizitaja zingine kuwa ni Mlandege (Iringa Mjini), Mdoe (Handeni Mjini), Sinza (Ubungo), Kisongo (Arumeru Magharibi), Uhuru (Dodoma Mjini), Bunju (Kawe), Kwa Kilosa (Iringa Mjini) na Kimbiji (Kigamboni).

Taarifa hiyo ilitaja zingine kuwa ni Msambweni (Tanga Mjini), Nsalala (Mbeya Vijijini), Nzuguni (Dodoma Mjini), Madukani (Dodoma Mjini), Kerege (Bagamoyo), Kibaoni (Kilombero), Kolo (Kondoa Mjini), Lumemo (Kilombero), Melela (Mvomero), na rufani mbili za kata ya Moivo (Arumeru Magharibi).

Kwenye taarifa hiyo, NEC ilisema imekataa rufani za wagombea udiwani ambao hawakuteuliwa, rufani ambazo zilitoka Kata za Duru (Babati Vijijini), Nundu (Nyang'wale), Magugu (Babati Vijijini) na Sangamwalugesha (Maswa Mashariki).

Ilizitaja zingine kuwa ni Pongwe (Tanga Mjini), Mpandangindo (Peramiho), Mji Mwema (Kigamboni), Kinampanda (Iramba Magharibi), Mbelekese (Iramba Magharibi), Maendeleo (Mbeya Mjini), Nalasi Mashariki (Tunduru Kusini) na Nyakabindi (Bariadi).

Kwa mujibu wa NEC kata zingine ni Nzovwe (Mbeya Mjini), Ndulungu (Iramba Magharibi), Kwediyama (Handeni Mjini), Kyengege (Iramba Magharibi), Kisisiri (Iramba Magharibi), Maluga (Iramba Magharibi), na Ndago (Iramba Magharibi).

Taarifa ya NEC ilisema kuwa imekataa rufani sita za kupinga wagombea udiwani walioteuliwa kutoka kwenye kata za Kisanga (Kalambo), Mwigobero (Musoma Mjini), Kirima (Moshi Vijijini), Gangilonga (Iringa Mjini), Majengo (Mbeya Mjini) na Lipangalala (Kilombero).

Taarifa hiyo ilisema idadi hiyo inafanya jumla ya rufani za wagombea udiwani zilizotolewa uamuzi kufikia 244 na kwamba itaendelea kutoa matokeo baada ya usajili na uchambuzi wa rufani hizo kila siku na wahusika watajulishwa na tume kwa barua kuhusu uamuzi uliofikiwa.


## NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Sisi **Tausi Auction Mart & Court Broker Co. Ltd** na **Adili Auction Mart Ltd** Kwa idhini tuliyopewa na **AMANA BANK LTD** na mamlaka tulionayo kisheria tunatoa notisi ya siku 14 kuanzia siku ya tangazo hili kwa wadaiwa wote na wadhamini mlipe madeni yenu yote kinyume cha hapo tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa wake. Mnada utafanyika mahali ilipo dhamana.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA NA MAHALI ILIPO**

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA INAYOUZWA | MAHALI DHAMANA ILIKO | TAREHE YA MNADA NA MUDA | MUUZAJI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | HANS WORLDWIDE SERVICES LIMITED | C.T No. 165557 L.O No. 552697 | Plot No 1360, Block 'C' Mtoni Kijichi Area, Temeke Municipality | Tarehe 03.10.2020 Saa 4:00 asubuhi na kuendelea | Tausi Auction Mart & Court Broker Co. Ltd Mawasiliano 0719351040 |
| 2 | HANS WORLDWIDE SERVICES LIMITED | C.T No. 165262 L.O No. 717104 | Plot No 1361, Block 'C' Mtoni Kijichi Area, Temeke Municipality | Tarehe 03.10.2020 Saa 4:00 asubuhi na kuendelea | Tausi Auction Mart & Court Broker Co. Ltd Mawasiliano 0719351040 |
| 3 | MWALULAS GENERAL SERV. & SUPPL. CO.(T) LTD | C.T No. 86064 L.O No. 397139 | Plot No 157, Block 'F' Ukonga Area, Ilala Municipality | Tarehe 02.10.2020 Saa 4:00 asubuhi na kuendelea | Adili Auction Mart Mawasiliano 0767873988 |

**MASHARTI YA MNADA**

1) Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
2) Ukaguzi wa dhamana utafanyika siku nne kabla ya mnada kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana.
3) Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine zikiwemo usafiri ni za mnunuzi.
4) Dhamana itauzwa "**kama ilivyo**"

**WOTE MNAKARIBISHWA**

215900402

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:**

MKURUGENZI MTENDAJI,
AMANA BANK LTD,
GOLDEN JUBILEE TOWER, 2ND FLOOR
S.L.P 9771,
**DAR ES SALAAM**

MKURUGENZI MTENDAJI, AU
TAUSI AUCTION MART & COURT BROKER CO. LTD,
MAGOMENI MIKUMI
S.L.P 71418,
**DAR ES SALAAM**

MKURUGENZI MTENDAJI,
ADILI AUCTION MART LTD,
MNAZI MMOJA
S.L.P 40616,
**DAR ES SALAAM**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kumaliza vichwa vikubwa kuko ndani ya uwezo wetu

TATIZO la watoto kuzaliwa na vichwa vikubwa na mgongo wazi linaelekea kuwa changamoto nyingine kubwa kwa sekta ya afya kutokana na kinamama wengi kujifungua watoto wenye tatizo hilo.

Wataalamu wa afya ya mifupa na mishipa ya fahamu wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), wanaeleza kuwa wastani wa watoto 700 hadi 1,200 hupokelewa kwa mwaka.

Wengine wana vichwa vikubwa na mgongo wazi na kueleza kuwa chanzo cha matatizo ni lishe duni kwa mama wakati wa ujauzito.

Lishe duni inatajwa kuwa ndicho chanzo cha kuzaliwa watoto wakiwa na aina hiyo ya ulemavu unaoumiza ubongo na mfumo wa fahamu na kwamba changamoto hiyo kwa kiwango kikubwa na mwaka jana watoto waliofika MOI kwa matibabu ya vichwa vikubwa walikuwa 886, kati yao 174 wakiwa na vichwa vyenye maji na mgongo wazi ni 69.

Tatizo linalowakabili kinamama wajawazito au wale wanaotarajiwa kuwa na hali hiyo ni ukosefu wa mlo wenye virutubisho vya folic ambavyo husaidia kuimarisha mishipa na mfumo wa fahamu na ubongo.

Lishe iko ndani ya uwezo wetu, ndiyo maana tunawakumbusha kula maharage, njegere, dengu, machungwa, juisi ya machungwa, brokoli, mboga za majani hasa spinachi, mchicha, matembele na kwa ujumla vyakula vyenye chuma.

Kikubwa hapa ni lishe jambo ambalo lipo ndani ya uwezo wa wahusika, hivyo cha msingi ni kuwaelimisha na wakatumia vyakula vinavyotakiwa ili kuepuka tatizo hilo.

Maparachichi, machungwa, mapapai, maembe, kabichi, maharage mekundu, majani ya maboga, choroko, mbaazi za kijani, mchicha, mayai na mihogo ya kuchemshwa, vinatajwa kuzuia ugonjwa huo.

Aidha, vitamini ya foliki inapatikana katika vyakula vya vitamini B na husaidia kuzuia kuzaa watoto wenye matatizo hayo, hivyo elimu ni muhimu kwa wazazi na pia kuhudhuria kliniki.

Mgongo wazi ni kichwa wazi ni matokeo ya kuathirika mishipa ya fahamu. Mgongo unakuwa na hitilafu hiyo kwa sababu unashindwa kujifunga kikamilfu kutokana na lishe duni wakati wa ujauzito na kusababisha mishipa kurundika na kuwa na umbo la nundu mgongoni.

Yote hayo yanasababisha kuumizwa kwa mishipa ya fahamu na uti wa mgongo licha ya kwamba MOI itafanya upasuaji na kuboresha maumbile yaliyoharibika lakini uharibifu wa mishipa ya fahamu ni wa kudumu na unakuwa na athari kwenye maisha ya watoto.

Tunaona kuwa athari za mishipa ya fahamu hazirekebishiki kikamilifu. Huathari kiakili ndiyo maana wengi wanaopata tatizo hilo huenda wakashindwa kujisoma na kuwa na uwezo kiakili, matatizo ya kupata haja na changamoto nyingine zinazohusiana na mwili kuwa na uhimilivu kutokana na hali tete ya uti wa mgongo.

Ni wito wetu kwa kinamama wajawazito na walio na matarajio ya kupata ujauzito kuwa na lishe bora, kufika kliniki mwezi wa kwanza wa ujauzito na kutumia dawa zenye madini ya chuma kwa ushauri wa daktari.


Tunatambua juhudi ambazo hufanywa na madaktari kusaidia watoto hao, lakini ni vyema sasa kinamama kuelimishwa jinsia ya kuepuka kujifungua watoto wenye matatizo ya aina hiyo.

Kama wataalamu wanavyoeleza kichwa kikubwa na mgongo wazi ni tatizo linalosababishwa na mfumo wa maji unaozunguka ndani ya kichwa kupata hitilafu hali ambayo husababisha maji kwenda kuziba mishipa yake na hatimaye kufanya kichwa kuwa kikubwa.

Lakini ni vizuri kinamama na wanajamii wakaachana na mazoea ya kukimbilia kwa waganga wa kienyeji wanapoona watoto wana matatizo hayo kwani sangoma wanayakuza badala ya kuyamaliza na kusababisha athari kubwa zaidi kimaisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wajasiriamali ni sawa biashara, vipi usafi nao?

Na Christina Mwakangale

KATIKA maeneo yenye mikusanyiko ndiko kuliko na fursa nyingi kuanzia za kibiashara hadi za kisiasa, ndiyo maana wajasiriamali wengi wanapatikana maeneo ya sokoni, vituo vya mabasi vya mijini na majijini, njiapanda, kando ya barabara, viwanja vya michezo, shuleni na hata ufukweni.

Wafanyabiashara hawa ambao ni wajasiriamali wadogo, huuza vyakula, vinywaji, mavazi na bidhaa za nyumbani, ambao pamoja na serikali kuwapa vibali kama vitambulisho vya kufanya biashara maeneo haya, kuna changamoto ya usafi na utunzaji wa mazingira yanayozunguka kazi zao.

Kwenye vituo vya daladala, mfano Makumbusho, Gongo la Mboto na Mbezi vilivyoko Dar es Salaam, utashuhudia taka na uchafu na kinachoonekana ni sawa na kusema kuwa hawajali wala kuzingatia usafi ila wanasaka pesa kwanza.

Pia, maeneo ya soko Tandika, Kariakoo, Manzese, Tandale na Buguruni hali ya uchafu ni hiyo hiyo na kwa ujumla masoko hayo hayapendezi machoni. Mtu ni afya, kuzitunza afya za wateja na unayeuza bidhaa ni kitu muhimu.

Ingekuwa ni bora fursa iendane na wajibu, sababu nafasi wamepewa wajasiriamali hawa ambao kundi kubwa ni vijana, siku hizi Kiswahili cha mjini wanasema 'kujiongeza', jiongezeni kwenye usafi.

Wafanyabiashara mjiongeze katika maeneo yenu kwa kila mmoja kuwa na ndoo au kapu la kutunza takataka zinazotokana na bidhaa mnazouza, si sawa hata kidogo uzalishe uchafu kwenye biashara zako kila dakika usubiri watu waje kukufagilia.

Kuna ambao watasema tunalipa ushuru. Ni sawa ushuru unalipwa, lakini akija mfanya usafi akute pa kuanzia, ikiwezekana taka zimetunzwa mahali fulani azikusanye na kumalizia kufagia.

Ni sawa na ukilipia ushuru, uache eneo chafu au mazingira machafu. Mbona katika vyoo vya kulipia utalipia ushuru wa Sh. 300 hadi 500 lakini baada ya kutumia choo iwe haja ndogo au kubwa utamwagia maji? Ni wachache wasio na uelewa wakaacha choo kichafu na kumfanya anayekuja nyuma yake arudi nyuma kama ameona chatu chooni.

Vivyo hivyo, hata wanaokuja kufanya usafi katika maeneo yenu ya biashara iwe soko au vituo vya daladala ni watu kama wengine, ambao wanahitaji kukuta utaratibu uliowekwa na wewe mzalisha uchafu kisha zikabebwa na gari taka hadi dampo.

Kituo pekee cha mfano wa kuigwa ni Simu 2000 au maarufu Mawasiliano kilichoko Dar es Salaam, kutokana na kupiga marufuku biashara katika kituo hicho.

Ni vyema wajasiriamali, wafanyabiashara kuweni rafiki wa mazingira kwa kuwa wasafi na pia wekeni vyombo vya kuhifadhia taka ngumu na si kuzitupa ovyo mitaroni barabarani.

Hii inawachanganya wafagizi wa barabara, ambao hutumia matoroli, ufagio na koleo, ili kuzoa mchanga akishafagia, huchanganyikiwa anakutana na maganda ya miwa, ndizi au chupa za maji yote hufanyakazi kuwa ngumu zaidi, kwani analazimika kuzoa mchanga na taka ngumu.

Wafanyabiashara hiyo ndiyo ajira isiyo rasmi, lakini inatambulika kwa kuziwezesha familia zenu kupata mahitaji na ni maendeleo pia kwa nchi, lakini kumbukeni mtu ni afya na maofisa afya na wajumbe wa kamati za afya na mazingira kwenye sehemu zao waongeze usimamizi, ufuatiliaji na kuchukua hatua kwa vile kama hamtaziba ufa mtajenga ukuta.

Kuna kipindi zilianza kampeni za kuwa na utaratibu wa kutumia sheria ndogo ndogo utakaowezesha kuwatoza faini wanaochafua mazingira ikiwa ni pamoja na kutupa taka ovyo na wanaojisaidia haja ndogo. Wakosaji wangelipishwa Sh. 50,000 papo kwa papo, mikakati hiyo iliishia wapi? Kama inawezekana kuna sababu ya kuangalia upya suala la tozo za papo kwa papo.

# Serikali yamega ranchi zake, yagawia wakulima, wafugaji

Na Ashton Balaigwa, MOROGORO

SERIKALI imemega maeneo kutoka katika mashamba na ranchi zake mikoani na kuwapatia wananchi waliovamia maeneo hayo ili waweze kuendeleza shughuli za kilimo, ufugaji na makazi ikiwa ni juhudi za kutatua migogoro ya wananchi na kulinda maeneo yaliyohifadhiwa kwa misitu na wanyamapori.

Kauli hiyo imetolewa na Victor Mwita, kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wakati akiwasilisha mada kwa waandishi wa habari wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET), yaliyofanyika kwa njia ya mtandao chini ya Ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID).

Mwita, alisema kuwa wizara hiyo, katika Mkoa wa Ruvuma, imemega hekta 1,800 kutoka katika shamba la Hanga Ngadinda na kuvipatia vijiji vya Gumbirona na Ngadinda huku pia ikimega eneo la hekta 2,208 kutoka Ranchi ya Ruvu na hekta 3,139 kutoka kituo cha Karantini cha Kwala na kuvipatia vijiji jirani ambavyo vimevamia maeneo hayo ya serikali.

Alivitaja vijiji vilivyomegewa eneo la Ranchi ya Ruvu kuwa vipo Wilaya ya Bagamoyo ambavyo ni Ruvu Darajani (hekta 200), Kidogozero (hekta200), Kitonga (hekta 480), Magulumatali (hekta200), Vigazwa (hekta8). Katika Wilaya ya Kibaha, vijiji vilivyomegewa eneo Mperamumbina (hekta 600), Kidomole (hekta 40), Fukayosa (hekta 40), Mkenge (hekta 40) na Milo (hekta 400).

Mwita alivitaja vijiji vilivyomegewa ardhi kutoka Kituo cha Karantini Kwala, kuwa ni vya wilaya za Kibaha ambavyo ni Dutumi (hekta 1,600) Madege (hekta 400), Kwala (hekta 400), Mwembengozi (hekta 400) na eneo la Mkuza Chicks (hekta 179.2), huku kwa upande wa Wilaya ya Bagamoyo, Kijiji cha Visegi -Kitongoji cha Kisogo kilipatiwa (hekta 160), lengo ni kuhakikisha rasilimali za misitu na wanyamapori zinalindwa kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Akizungumzia wafugaji, alisema katika kuhakikisha wanapata maeneo ya malisho kwa ajili ya mifugo yao, wizara hiyo imetenga hekta 48,502.2 kutoka kwenye Ranchi za Taifa na kuwapatia wafugaji kwa utaratibu maalumu na muda mfupi.

Alizitaja ranchi zilizotenga maeneo hayo ni pamoja na Kongwa (hekta 13,591.7), Kalambo (hekta 10,000.0), West Kilimanjaro (hekta 2,416.0), Kikulula (hekta 7,381.6), Misenyi (hekta 10,049.2), Mabale (hekta 1,950.0) na Kigoma (hekta 3,113.7).

Kwa upande wake Dk. Stephen Nindi kutoka Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (NLUPC), alisema kuwa tayari wameshaainisha maeneo mbalimbali ya shughuli zote za rasilimali za ardhi ikiwamo maeneo ya malisho, ufugaji, kilimo na makazi huku vijiji vyote vikitakiwa kutengeneza mipango ya matumizi ya ardhi kupunguza migogoro inayojitokeza kati yao hifadhi za misitu na wanyamapori.

Mkurugenzi wa JET, John Chikomo, alisema lengo la mafunzo hayo kwa njia ya mtandao ni kusaidia serikali kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya uhifadhi wa mazingira na wanyamapori nchini, ili serikali iweze kufikia malengo yake ikiwamo kuondokana na tatizo la ujangili.




Mwonekano wa nje wa sehemu ya jengo la machinjio ya kisasa ya Vingunguti, Manispaa ya Ilala, jijini Dar es Salaam jana, likiwa katika hatua za mwisho za ujenzi unaofanywa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Ujenzi hospitali Uhuru Dodoma wafikia 87%

Na Mwandishi Wetu

UJENZI wa Hospitali ya Uhuru wilayani Chamwino mkoani Dodoma, imekamilika kwa asilimia 87 baada ya serikali kutekeleza ahadi yake ya kuzielekeza takribani Sh. bilioni 2.3 zilizotolewa na Kampuni ya Bharti Airtel ya India kujenga hospitali hiyo.

Hayo yalibainishwa na Mhandisi wa Ujenzi wa jengo la Hospitali ya Uhuru, Girimu Kanansi, wakati Ofisa Mawasiliano wa Airtel Tanzania, Jackson Mmbando, alipotembelea hospitali hiyo kuangalia maendeleo ya ujenzi wake.

Alisema kuwa jengo hilo lililokamilika kwa asilimia 87 linajengwa kwa weledi mkubwa na Kampuni ya Suma JKT kupitia vijana wazalendo wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), kinyume na awali ambapo majengo makubwa kama hayo yalikuwa yanajengwa na kusimamiwa na wageni kutoka nje ya nchi.

"Kazi inayoendelea ni kutengeneza sakafu, kuweka mifumo ya umeme na kuskimu kuta, hivyo ninaishukuru serikali na Kampuni ya Mawasiliano ya Airtel kuona umuhimu wa kupeleka huduma za afya karibu na wananchi hususani mkoani Dodoma ambako ndio makao makuu ya nchi," alieleza Mhandisi Kanansi.

Alisema jengo hilo lilitarajiwa kukamilika Mei mwaka huu, lakini ilishindikana kutokana na changamoto ya msimu wa mvua ambao ulisababisha kutokuwa na mazingira rafiki ya kusafirisha vifaa kwenda eneo la ujenzi.

Aidha, kutokana na hali hiyo, mkandarasi aliomba kuongezewa muda, ambapo anatarajia kukamilisha ujenzi Oktoba mwaka huu iwapo hakutakuwa na changamoto yoyote itakayojitokeza ikiwamo ya kutofika kwa vifaa vya ujenzi kwa wakati.

Kwa upande wake Mbando alisema kampuni hiyo imekuwa na utaratibu wa kutembelea eneo hilo la ujenzi kuona maendeleo yake kwa kuwa ni sehemu ya kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema baadhi ya miradi ni ya afya ikiwamo Hospitali ya Uhuru ambayo kupitia mbia mwenza Bharti Airtel ya Tanzania ndio iliyotoa kiasi cha Sh. bilioni 2.3 kwa serikali ambayo ilizielekeza katika ujenzi wa hospitali.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa Kampuni ya Airtel Tanzania ikitoa gawio kwa serikali, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Doto James, alisema Serikali ya Tanzania ilianza uchunguzi wa umiliki wa Airtel Tanzania na baadaye kufanya mazungumzo na Kampuni mama ya Bharti Airtel ya India kuanzia mwaka 2018 na kufanikisha serikali kumiliki asilimia 49 ya hisa za kampuni hiyo.

Alisema makubaliano hayo yaliyosababisha kunufaika kwa pande hizo mbili ndiyo yalimfanya Mwenyekiti wa Bharti Airtel ya India, Sunil Mittal, kutoa Sh. bilioni 2.3 kwa serikali ikiwa ni shukrani kwa kuanza makubaliano mapya yenye tija.

## 400 waliosoma nje kukutanishwa

Na Joseph Mwendapole

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye mahafali ya pili ya kimataifa kwa wanafunzi waliosoma nje ya nchi yanayotarajiwa kufanyika mwishoni mwa wiki Mlimani City, jijini Dar es Salaam.

Mahafali hayo yanayotarajiwa kuwakutanisha wanafunzi 400 waliosoma vyuo vikuu mbalimbali nje ya nchi kupitia Taasisi ya Elimu nje ya nchi ya Global Education Link (GEL).

Mkurugenzi wa GEL, inayowaunganisha wanafunzi na vyuo vikuu nje ya nchi, Abdulmalik Mollel, wakati akizungumza kwenye kikao cha maandalizi ya mahafali hayo.

Alisema lengo la mahafali hayo ni kuhakikisha wanafunzi Watanzania waliosoma nje ya nchi hawarudi kimya kimya na kinyonge kwa kuwa wao ni wazalendo walioamua kuacha fursa zilizoko huko baada ya masomo yao na kuja kuijenga nchi yao.

Mollel alisema wahitimu hao waliaminiwa na taifa na ndiyo sababu walipewa viza za kwenda kusoma nje ya nchi kwaajili ya manufaa yao familia zao na kwaajili ya nchi yao hivyo kurudi kwao ni kurejesha furaha nyumbani kwani wanatarajiwa kutoa mchango mkubwa kwa nchi.

Alisema GEL itawakutanisha wanafunzi hao kwa ajili ya kujenga mtandao na taasisi na watu mbalimbali hapa nchini baada ya kukaa nje ya nchi kwa muda mrefu ambako huko walishajenga aina nyingine ya maisha.

"Mfano mtoto ameenda huko akiwa na miaka 17 amekaa huko miaka minne au sita anarudi amekuwa mtu mzima amekuta mambo mapya sasa akifika akikosa timu kama aliyokuwa nayo kule anakata tamaa sasa kitendo cha kumkutanisha mtu aliyekuwa Uingereza, India, China, Canada au Afrika Kusini kwenye jengo moja ni jambo kubwa sana na la msingi," alisema Mollel.

Alisema wanafunzi hao wakikutanishwa wataona kama milango ya maisha yao imefunguliwa kwa kuwa watatengeneza mtandao mpya na wenzao waliomaliza nao mwaka mmoja kwenye vyuo hivyo nje ya nchi kwasabu awali hakukuwa na mahafali ya aina hiyo.

Kwa mujibu wa Mollel, mahafali hayo ni fursa kwa wahitimu hao kwa kuwa kuna kampuni mbalimbali ambazo zimetoka kwenye nchi nyingine ambazo wanafunzi hao walisoma zitakuwa zinatafuta wataalamu wa fani wanazozihitaji hivyo wakikutanishwa itakuwa na manufaa kwao.

"Kuna wawekezaji ambao wanatafuta watu waliosoma kwenye nchi zao angalau wenye kujua lugha zao kidogo sasa hii ni nafasi ya kuwaita hawa kwamba nani amewekeza nini na anahitaji vijana wataalamu sasa ukiwakutanisha ni fursa kubwa sana kwa wawekezaji na vijana," alisema Mollel.

**"Mfano mtoto ameenda huko akiwa na miaka 17 amekaa huko miaka minne au sita anarudi amekuwa mtu mzima amekuta mambo mapya sasa akifika akikosa timu kama aliyokuwa nayo kule anakata tamaa sasa kitendo cha kumkutanisha mtu aliyekuwa Uingereza, India, China, Canada au Afrika Kusini kwenye jengo moja ni jambo kubwa sana na la msingi," alisema Mollel.**

# Majaliwa awaomba Kondoa kuiamini CCM

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wananchi wa Kondoa waendelee kuwaamini viongozi wanaoletwa na CCM ili walete maendeleo zaidi.

"Endeleeni kuiamini serikali hii ili iendelee kuongoza, endeleeni kuwaamini viongozi wanaoletwa na CCM ili waendelee kuleta maendeleo zaidi. Ninaomba kura za Mheshimiwa Rais, wabunge na madiwani watarajiwa sababu ndiyo wataleta maendeleo katika maeneo yenu," amesema.

Alitoa wito huo juzi wakati akizungumza na wananchi wa Kondoa Mjini na Vijijini waliofika kusikiliza sera za wagombea kwenye uwanja wa Sabasaba, wilayani Kondoa, mkoani Dodoma.

Majaliwa ambaye alifika wilayani humo kumwombea kura Rais John Magufuli na wagombea ubunge wa Kondoa Mjini, Ally Makoa na Dk. Ashatu Kijaji wa Kondoa Vijijini na wagombea udiwani wa CCM, aliwataka wananchi hao watumie kipindi hiki kutafakari kwa kina na kuchagua viongozi wanaowafaa.

"Wananchi msiyumbe, tuna uchaguzi wa aina mbili. Uchaguzi wa kwanza ni kuchagua kiongozi anayeweza kuleta maendeleo na mwenye uwezo wa kuleta maendeleo na uchaguzi wa pili ni uchaguzi wa kishabiki wa kufuata upepo. Tutumie kipindi hiki kichagua viongozi wanaoweza kutusemea masuala la maendeleo," alisema.

Kuhusu miundombinu ya barabara, Majaliwa alisema serikali imefanikiwa kuunganisha makao makuu ya mikoa kwa barabara za lami na hata katika baadhi ya wilaya, huku akitolea mfano wa kutoka Babati hadi Kondoa, Kondoa hadi Chemba na Chemba hadi Dodoma.

"Sasa hivi tunataka kufungua barabara ya kutoka Babati hadi Orkesumet, na hii ya kutoka Handeni - Kiberashi - Kondoa - Singida iko kwenye Ilani yetu ya sasa ukurasa wa 73. Barabara hii ikitoka Handeni itapita Kilindi - Kiteto - Kondoa hadi Singida."

Katika barabara za wilaya, Majaliwa alisema hizo zinashughulikiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ambao wamepatiwa Sh. bilioni 1.840 na Sh. bilioni 6.4 nyingine zilitolewa kwa ajili ya barabara za Kondoa vVijijini kutoka makao makuu na kuunganisha kata hadi kata.

Kuhusu mikakati ya serikali ya kukuza uchumi, alisema kuna watu wanabeza ujenzi wa reli na ununuzi wa ndege, lakini wanasahau kuwa maendeleo hayaji bila maendeleo ya vitu. "Huwezi kupata maendeleo ya watu bila kuwa na maendeleo ya vitu," alisisitiza.

Kwenye sekta ya kilimo, Majaliwa alisema wananchi wa Kondoa ni wakulima wazuri wa mazao mbalimbali na akawakumbusha wakazi hao jinsi ambavyo serikali imeboresha upatikanaji wa mbolea na pembejeo za kilimo.



Mafundi wakiendelea na ukarabati wa barabara ya TRA, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuharibika kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo. **PICHA: FRANK MAXMILLIAN/TUDARCo**

# Wafugaji kupeleka maziwa nje ya nchi

**Na Renatha Msungu, ARUSHA**

WAFUGAJI kutoka Kanda ya Kaskazini wamepata kibali cha kupeleka maziwa nje ya nchi, jambo ambalo litawezesha kupata kipato zaidi na kuondokana na ukosefu wa masoko.

Akizungumza na waaandishi wa habari Mkurugenzi Mtendaji wa Kilimanjaro Fresh, Irfhan Virjee, alisema wanatarajia kuanza kupeleka maziwa nchini Kenya kama moja ya upanuzi wa soko la maziwa.

"Tunakaribia kuanza kupeleka maziwa nchini Kenya lengo ni kupanua soko la wafugaji wetu hapa nchini," alisema.

Alisema hivi sasa kiwanda chao kinakusanya maziwa kiasi cha lita 10,000, lakini matarajio yao ni kukusanya lita 72,000 ambazo zitajitosheleza katika usambazaji.

Kwa Mujibu wa Mkurugenzi huyo, wamejipanga kutembelea wafugaji ili kuhakikisha wanapata maziwa ya kutosha katika nchi za jirani kwa ajili ya kukuza soko.

Alisema kupitia bidhaa za Kilimanjaro Fresh wafugaji wengi wamenufaika kutokana na soko lao kuwa pana ambapo hivi sasa wafugaji wataanza kunufaika na soko hilo.

Alisema wamejipanga kuhakikisha soko linakua na wafanyabiashara ya maziwa watanufaika sana kutokana na upanuzi wa soko ndani na nje ya nchi.

Naye Mdhibiti ubora wa Kilimanjaro Fresh, Subira Shabani, alisema maziwa kabla ya kupelekwa sokoni ili kuhakikisha kila yanapokwenda yanakuwa salama kwa walaji.

Subira alisema maziwa yanayosambazwa na Kilimanjaro Fresh yana soko kubwa ndani na nje ya nchi.

"Tumejipanga kuhakikisha bidhaa zinakuwa bora na soko linakuwa kubwa kutokana na umaridadi wa maziwa waliokuwa nayo," alisema Subira.

Naye mfugaji Lukumay John, alisema kabla ya kiwanda cha Kilimanjaro Fresh wafugaji walikuwa wakipata hasara kutokana na maziwa kuharibika.

Alifafanua zaidi ya kuwa hivi sasa maziwa hayawasumbui tena kutokana na kiwanda hicho kukusanya lita 10,000 za maziwa kutoka kwa wafugaji na kwamba wafugaji hivi sasa hawana shida yoyote kuhusiana na soko la maziwa ambayo awali ilikuwa ni changamoto kubwa.

# Mambo 10 kuyafanyia kazi akichaguliwa

**Na Augusta Njoji, MANYONI**

MGOMBEA wa Jimbo la Manyoni Mashariki kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Pius Chaya, ametaja mambo 10 atakayoyasimamia endapo akichaguliwa, ikiwamo kujenga jengo kwa ajili ya wajawazito wanaosubiri kujifungua maarufu kama Chikande, ambao kwa sasa wanatumia ghala la tumbaku.

Akizungumza jana kwenye uzinduzi wa kampeni za jimbo hilo, Dk. Chaya alisema, amefanya tathmini kuwa ujenzi wa jengo hilo utagharimu Sh. milioni 60 hivyo akichaguliwa atahakikisha anaondoa tatizo hilo, ili kinamama hao wakae kwenye jengo linalokidhi viwango.

Aliahidi akichaguliwa, atasimamia ujenzi wa hospitali ya wilaya kwa kuwa iliyopo ilipandishwa hadhi kutoka kituo cha afya na hivyo kuwa na msongamano wa wagonjwa.

"Sitaishia kwenye hospitali, nitahakikisha tunasogeza huduma za afya kwa wananchi kwa kujenga zahanati na vituo vya afya, ili wananchi wetu muondokane na tatizo la kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya," alisema.

Kuhusu maji, Dk. Chaya alisema atahakikisha akichaguliwa ndani ya mwaka mmoja tatizo hilo linakuwa historia kutokana na kuwapo kwa mradi mkubwa utakaotekelezwa kwenye jimbo hilo.

Akizungumzia sekta ya elimu, alisema kuna tatizo la baadhi ya shule za sekondari na msingi ambazo hazijasajiliwa na kuahidi kuzifuatilia, ili zipate usajili na kuondoa tatizo la wanafunzi kutembea umbali mrefu, kufanya mitihani kwenye shule zilizosajiliwa.

"Najua kwenye Shule ya Sekondari Sasilo, Salanda hazijasajiliwa, ikifika wakati wa mitihani watoto wanatembea kwenda kufanya kwenye shule zilizosajiliwa, hili linahitaji ufuatiliaji na mimi ndio nguli kwenye masuala ya ufuatiliaji, nitahakikisha zinasajiliwa," alisema.

Dk. Chaya alisema, kwenye kilimo na mifugo atahakikisha anainua sekta hiyo kwa kuhakikisha kunakuwapo na mabwawa na majosho.

Kuhusu tatizo la ajira, alisema akichaguliwa atahakikisha anawatambua wahitimu wote, kuwajengea ujasiri wa kutafuta ajira na kuwasaidia waajiriwe.

"Pia nitahakikisha naibadilisha Manyoni kwa kuweka taa za mitaani kwenye maeneo yaliyochangamka," alisema.

Vile vile, aliahidi kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Manyoni kukomesha vitendo vya uhalifu kwa kuongeza askari na kujenga vituo vya polisi.

Kwa upande wake, aliyekuwa Mbunge wa jimbo hilo, Daniel Mtuka, alisema anamwamini mgombea huyo ataongoza vyema na kuchochea maendeleo kwa kasi ya jimbo hilo zaidi yake.

Naye Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, Munde Tambwe, aliwaomba wananchi kuhakikisha wagombea wote wa CCM wanapata ushindi wa kishindo kutokana na mafanikio yaliyofanywa na serikali ya awamu ya tano.

# Bima ya afya kuwakomboa wakulima

**Na Mwandishi Wetu**

HUDUMA ya bima ya afya kwa wakulima walio katika mfumo wa vyama vya ushirika imezinduliwa rasmi, hatua ambayo itawawezesha kuwa na uhakika wa matibabu kulingana na makubaliano waliyoingia.

Mfuko wa Bima ya Taifa ya Afya (NHIF) umezindua huduma hiyo kwa wakulima, kupitia mpango wa ushirika afya, itatolewa kwa kushirikiana na Benki ya Posta (TPB).

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema mkulima kupitia vyama vyao vya msingi atachangia Sh. 76,800, wakati mwenza wake atachangia Sh. 76,800, wakati watoto chini ya miaka 18 watachangia Sh. 50,400 kwa mwaka.

Mkulima akishapewa kadi yake ya bima atanufaika na huduma kadhaa ikiwamo kumuona daktari, huduma ya dawa, vipimo, wagonjwa wa nje na kulazwa, upasuaji mdogo na mkubwa, miwani ya kusomea, afya ya kinywa na meno, mazoezi ya tiba ya viungo na tiba ya macho.

**Kwa sasa mpango huu wa huduma ya afya kwa wakulima, umeanza na mazao ya kimkakati hususani zao la pamba, ambalo linalimwa zaidi kanda ya ziwa.**

Akizindua huduma hiyo juzi, Mkuu wa Mkoa Tabora, Dk. Philemon Sengati, aliwataka wakulima kujitokeza na kuitumia fursa hiyo vizuri kwa kuwa itasaidia kuchochea ufanisi katika uzalishaji mazao, hivyo kujiinua zaidi kimapato na kufanikiwa kupata maendeleo.

Huduma hiyo ilizinduliwa katika kijiji cha Mwamashimba kilichopo Wilaya ya Igunga, alibainisha kuwa mkulima atakajiunga na huduma hiyo atakuwa na amani ya kumudu gharama za matibabu, hivyo mapato yake mengi yatatumika kwa maendeleo zaidi.

"Wakulima ni kundi ambalo lilisahaulika katika upatikanaji wa huduma ya afya nchini, hivyo napenda kuishukuru TPB na NHIF kwa kukumbuka kundi hilo, ni vyema kwa taasisi nyingine za serikali ziweze pia kuiga mfano mashirika haya mawili," alisema.

Makubaliano ya kuanza kwa huduma hii yanahusisha pande tatu, ambazo ni Benki ya TPB, Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) na vyama vya ushirika katika Kanda ya Ziwa.

Mpango huu umepangwa kuongeza vyama vingine vya msingi kama vile; Shinyanga Cooperative Union (SHIRECU), Kahama Cooperative Union (KACU), Simiyu Cooperative Union (SCU), Nyanza Cooperative Union (NCU) na vyama vingine vilivyopo kanda ya ziwa.

Vyama vya msingi vya ushirika kupitia ofisi ya mrajisi wa vyama vya ushirika nchini, vitaingia makubaliano na NHIF na TPB kwa kusaini makubaliano ya awali (mou) ya ufanyaji kazi kwa Kanda ya Ziwa, ambapo ndipo huduma hiyo itakapopatikana.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya TPB, Sabasaba Moshigi, alisema "Kwa sasa mpango huu wa huduma ya afya kwa wakulima, umeanza na mazao ya kimkakati hususani zao la pamba, ambalo linalimwa zaidi kanda ya ziwa."

Alisema, huduma hii ya bima ya afya kwa wakulima imeanza kwa majaribio katika Kanda ya Ziwa, ambapo zao la pamba linalimwa kwa wingi na majaribio ya huduma hii yanafanyika kwa kushirikiana na Chama cha Ushirika cha Igembensabo Cooperative Union, kilichopo Igunga-Tabora.

Meneja wa tawi la TPB mkoani Tabora, Timon Massawe, alisema kwa kupitia mpango huu benki hiyo itatanua wigo wa wateja, kufungua akaunti za vyama vya ushirika kwa ajili ya makusanyo ya bima na pia shughuli za uendeshaji wa vyama husika.



Mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Sauti ya Umma (SAU), Muttamwega Mgaywa (kulia), akisalimiana na Ofisa Mstaafu wa Jeshi la Polisi, mzee Ambwene Mwamakula, baada ya kumaliza kuhutubia mkutano wa kampeni eneo la Ukonga Mombasa, jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wazazi wataka mkazo masomo sayansi

**Na Frank Kaundula,** PWANI

WAZAZI wenye watoto wanaosoma katika Shule ya Sekondari Bwawani inayomilikiwa na Jeshi la Magereza nchini iliyoko Pwani, wamewataka walimu kutoa kipaumbele kwa masomo ya sayansi ili wanafunzi wafaulu kwa wingi.

Wazazi hao waliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa siku ya wazazi shuleni hapo, ambapo walikiri kuwa shule hiyo hufanya vizuri kitaaluma, lakini ni kwa masomo ya sanaa hivyo wakaomba pia masomo ya sayansi yahimizwe pia.

Acquviline Malisa, alisema shule hiyo imekuwa ikifanya vizuri kitaaluma kila mwaka kwa masomo ya sanaa hivyo kipaumbele kwa masomo ya sayansi kiongezwe ili vijana wao wafaulu vizuri.

"Mwaka huu mwanafunzi wa kwanza masomo ya sayansi kidato cha sita mchepuo wa CBG (Combination) alipata daraja la tatu, lakini masomo ya sanaa wanafunzi wengi wamefaulu kwa kupata daraja la kwanza na la pili," alisema Acquviline.

Alisema kutokana na ufaulu wa vijana wao kuwa chini kidogo tofauti ma wale wanaosoma mchepuo wa sanaa, kumekuwa kukisababisha wakose sifa ya kujiunga na elimu ya vyuo vikuu, hivyo jitihada zaidi inahitajika ili kutatua suala hilo.

Aidha, alipongeza uongozi wa shule hiyo ikiwa ni pamoja na Jeshi la Magereza kuhimiza nidhamu kwa wanafunzi wote ambapo alisema wazazi wataendelea kutoa ushirikiano ili kukuza taaluma na nidhamu katika shule hiyo.

Majura Tomas, alipongeza uongozi wa shule hiyo kuweka siku maalumu ya wazazi kukutana na watoto wao pamoja na uongozi wa shule, ambapo alisema kitendo hicho kinasaidia sana kutatua changamoto na kukuza taaluma.

Mkuu wa shule hiyo, Anthony Sogoseye, alisema kuwa ili kuhakikisha wanafunzi wa mchepuo wa sayansi wanafaulu vizuri mitihani yao ya taifa shule imeanzisha utaratibu wa kutenga muda wa ziada wa kuwafundisha.

Sogoseye alisema shule imeamua kutenga muda wa ziada ili walimu wa sayansi waweze kujitoa na kufundisha wanafunzi wa michupuo hiyo na kwamba vifaa vya maabara vimeboreshwa kwa lengo la kuongeza ufaulu wa wanafunzi.

Jeremiah Katungu, Naibu Kamishna wa Magereza, alipongeza nidhamu ya wanafunzi iliyopo ambapo aliwataka wazazi kulipa ada kwa wakati kuepusha usumbufu.

Kamishna huyo kutoka makao makuu ya jeshi hilo, alisema changamoto zote zilizopo katika shule hiyo zitafanyiwa kazi kadri iwezekanavyo kwani lengo ni kutaka kuona Bwawani Sekondari inakuwa shule ya mfano kitaifa na kimataifa.

# Ukuaji rasilimali watajwa kuipaisha Mkombozi

**Na Yasmine Protace**

BENKI ya Biashara ya Mkombozi imesema mafanikio makubwa yaliyopatikana mwaka jana yalitokana na ongezeko la ukuaji wa rasilimali.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Profesa Marcelina Chijoriga, katika mkutano wa 11 wa wanahisa wa benki hiyo, uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema, rasilimali zikiongezeka kwa asilimia 14, kutoka Sh. bilioni 278.8 Desemba 31, 2018 mpaka Sh. bilioni 204 Desemba 31, 2019.

"Mikopo na karadha kwa wateja iliongezeka kwa asilimia 23.3 kutoka shilingi bilioni 99 Desemba 31, 2018 mpaka shilingi bilioni 122 Desemba 31, 2019," alisema Profesa Chijoriga.

Aliongea kuwa, amana za wateja ziliongezeka kwa asilimia 18.7 kutoka shilingi bilioni 136 Desemba 31, 2018 hadi shilingi bilioni 162 Desemba 31, 2019.

Alisema, ada na kamisheni ilipanda kwa asilimia 30 kutoka shilingi bilioni 3.17 kama tarehe 31 Desemba 2018 mpaka shilingi bilioni 4.12 kama tarehe 31 Desemba 2019.

Aliongeza kuwa, benki ipo katika njia sahihi katika kutekeleza mipango mikakati muhimu ili kufanikisha ajenda yake kuu, ambayo ni ukuaji wa faifa endelevu.

"Baadhi ya mipango ni kuanzisha mfumo wa huduma za benki kwa njia ya wakala, matumizi ya teknolojia mpya katika utoaji wa kadi za ATM, ambao unawezesha utoaji wa kadi wa ATM, mteja akiwa kaunta mara tu baada ya mteja kufungua akaunti," alisema.

Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba 15, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

**Kijana anayetamani kusoma kusudi awasaidie wengine**



Ukurasa 13

Kwa taarifa, ukame ni chanzo cha maradhi kama ilivyo mvua



Ukurasa 14

**Wanafunzi sasa waingia vitani kupigana mimba, ndoa utotoni**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Mlipuko COVID-19 ulipotajwa kulipua mimba na ndoa utotoni

## ▪Ndoa za wanafunzi ni usiku wa manane
## ▪101 wapata ujauzito 'bye bye' shule

MLIPUKO wa COVID-19 ulioripotiwa nchini Machi mwaka huu, pamoja na kulazimisha shule kufungwa kwa miezi mitatu, unatajwa kuharibu mustakabali wa wasichana 101 mkoani Shinyanga, ambao wamepata ujauzito wakati wa likizo ya corona, huku wengine wakiozwa ndoa za utotoni.

Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ni miongoni mwa maeneo ambayo mabinti walipata ujauzito, katika kipindi cha corona na sasa imeibuka kazi nyingine ya ziada ya kutibua kila mara ndoa za wanafunzi.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wa halmashauri hiyo, Deus Mhoja, anasema hadi sasa ndoa za wanafunzi watatu zimetibuliwa na harakati zikiendelea kukwamisha mipango ya kuoza mabinti wanafunzi.

Anasema hata hivyo nyingine zinafungwa na mambo yote kumalizwa usiku wa manane, ili kuficha taarifa na kisha wanafunzi kutoroshwa na kuacha masomo.

"Ndani ya miezi miwili tumetibua ndoa tatu, ikiwamo nyingine ya mwanafunzi ambaye tayari alikuwa ameshajifungua mtoto mwenzie na nyingine ambayo tuliikatisha hivi karibuni Septemba 4 ya mwanafunzi wa kidato cha kwanza.

Huyo alikuwa akisoma Sekondari ya Mwantini, tukianza kwenye mkakati ulivyopangwa wa kumwozesha mwanafunzi huyo hadi kufikia hatua ya kumfungisha ndoa usiku," anasema Mhoja.



Wasichana wanastahili kuwa shuleni na kusoma siyo kuozwa utotoni na kukwamishwa kimaisha.**PICHA : MTANDAO.**

Anaeleza kuwa mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa) mwenye umri wa miaka 17, aliozwa kwa mahari ya Sh. milioni 1.5 yaliyoanza kutolewa alipofika darasa la saba walikuwa wakichukua nusu na alipofika kidato cha kwanza ilikamilika na kujipatia milioni 1.5 mapema mwezi huu.

Anafafanua kuwa baada ya mahari hiyo kukamilika, mwanafunzi alianza kuwa mtoro shuleni kabla ya janga la corona na shule zilipofungwa mambo yakaendelea, lakini zilipofunguliwa wazazi walimzuia kwenda shule, ili zifike siku 90 afukuzwe kwa utoro, ili wapate mwanya wa kumuozesha na kuzima ndoto zake.

"Wazazi wamekuwa chanzo cha mimba na ndoa za utotoni ambazo zinaendelea kushika kasi mkoani Shinyanga. Hawapendi kusomesha watoto wa kike ila kuwaozesha ndoa za utotoni bila ya kujali ni watoto wadogo tena mwanafunzi. Kinachowasukuma ni kupata pesa tu na mifugo," anasema Mhoja.

"Mfano ndoa hizi tulizozitibua, wazazi ndiyo wamepanga mikakati yote ya kuwaozesha wanafunzi. Na sisi tunachokifanya hivi sasa ni kuwakamata wahusika wa pande zote mbili, akiwamo na bwana harusi na kuwapeleka polisi, ili hatua zaidi za kisheria ziendelee kuchukuliwa dhidi yao," anaongeza.

Katika mkasa huo wa kumwozesha binti yao wa Septemba 4, 2020 ambalo lina ushahidi, wana familia wanaodaiwa kuhusina na ndoa hiyo (majina yanahifadhiwa) wanakiri kuwa walifanya hivyo.

Wahusika ambao wanashikiliwa na polisi kwa kumwozesha mtoto mwanafunzi, wanasema tatizo ni binti yao kutokujiweza kielimu.

Akizungumza na Nipashe mmoja wao, anasema aliamua kumwozesha mtoto wake huyo, baada ya kugundua hana akili darasani na kwamba amekuwa akifanya vibaya, huku akidai kuwa hata mtihani wa darasa la saba alifanyiwa ndiyo maana alifaulu hivyo hakuona haja ya kuendelea kumsomesha, bali wamtafutie mwanaume wa kumwoa.

"Ni kweli tumemwozesha binti yangu kwa mahari ya Sh. milioni 1.5 ni baada ya kuona hana akili tukaona bora tumtafutie mwanaume aolewe asije akapewa ujauzito na kuzalia nyumbani tukakosa mali," anasema mama mzazi wa binti huyo.

Mwanafamilia mwingine kwa upande wa bwana harusi ambaye yupo chini ya ulinzi wa polisi, anapozungumza na gazeti hili anakiri kufanya makosa ya kumuoza mwanafunzi, na kubainisha kuwa atafanya juhudi kushirikiana na polisi hilo, ili kumpata bwana harusi ambaye ametoroka na mwanafunzi huyo mara baada ya kumaliza kufunga ndoa usiku.

Sonda Kabeshi ni mzee na kiongozi wa mila wa Kijiji cha Mwatini, anasema kwa utamaduni wa wakazi wa eneo hilo unaruhusu mtoto wa kike kuachwa bila kusoma kwani anadaiwa kuwa akisoma ana kwenda kunufaisha ukoo alioolewa na pia ni vigumu kuolewa tena kwa sababu hata kuwa na heshima kwa mwanaume na hatamtii sababu ya elimu yake kubwa.

"Utamaduni wetu ni wa kizamani sana, siku hizi watoto wa kike wanasomeshwa na wanatusaidia tu vizuri, wanajituma kuhudumia familia zao kuliko hata wakiume

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA CHRISTINA HAULE, MOROGORO

SALUM PANDU

# Kijana anayetamani kusoma kusudi awasaidie wengine

SALUM Pandu anayeishi Kijiji cha Lubungo A, wilayani Morogoro, ana shauku ya kusoma zaidi, akilenga kufanikiwa ili awasaidie wana kaya na jamii wahitaji wanaomzunguka.

Kupitia mpango wa kusaidia kaya maskini unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) amepata elimu ya sekondari hadi kidato cha sita na sasa anatamani kuingia katika hatua nyingine, kwenda hadi chuo kikuu.

Anawaomba wadau wa elimu kumpa msaada wa kuendelea zaidi kielimu kumwezesha kutimiza azma yake ya kuzisaidia kaya za wahitaji na jamii inayomzunguka.

Salum mwenye miaka 24 anatoka katika familia ya watu watatu inayohudumiwa chini ya mpango wa kunusuru kaya maskini -TASAF III awamu I, anaishi na bibi yake Tabia Gombe (78) na dada Mwajuma Pandu. Kijana huyo alimaliza darasa la saba katika Shule ya Msingi Muungano mwaka 2013 na kusomeshwa na TASAF Sekondari ya Mikese ikimgharamia mavazi, ada na madaftari hadi alipomaliza 2016.

Aidha, alisoma kidato cha tano na cha sita katika Sekondari Namabengo mkoani Ruvuma akichukua mchepuo wa Historia Geografia na Fasihi (HGL) akigharamiwa na TASAF na kufaulu vizuri.

Kiu ya Salum ni kujifunza masuala ya maendeleo ya jamii au shahada ya ualimu na kuwaomba wadau kumsaidia kufikia malengo yake na lengo lake ni kusaidia na wengine wasio na elimu kuinuka hasa kwenye maeneo ya kijijini anakoishi.

**MAHITAJI ANAYOOMBA**

Anaomba Shilingi 26,000 za kuchukua, kujaza na kurejesha fomu ya mkopo, mavazi, malazi na ada awapo chuoni. Katika hili amepata msaada na baadhi ya waliojitokeza kumsaidia ni wanahabari waliotembelea kijiji cha Lubago A na kumchangia Shilingi 62,000 ili kujaza fomu ya mkopo.

"Nawashukuru wahariri na wanahabari kwa kunisaidia mara mbili nilichokuwa nahitaji, endeleeni kusaidia wengine ili wawasaidie jamaa zao na jamii kwa ujumla na mimi pia nitakaposoma nitaweza kusaidia wengine," anasema Pandu.

Aidha, Ofisa Ufuatiliaji wa TASAF Wilaya ya Morogoro Judith Waiso, anawaomba walengwa wa TASAF kutambua kuwa taasisi hiyo inawawezesha wanafunzi kupata mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) na kujiendeleza kielimu baada ya kujaza fomu ya utambulisho kutoka TASAF.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Huduma, Amedeus Kamagenge, anasema watoto wanaotoka katika kaya maskini ambazo inahudumiwa na TASAF ni rahisi kupata mkopo wa kujiendeleza kielimu.

Kamagenge anasema imewasaidia wamewasaidia wanafunzi 277 mwaka 2019 kujiendeleza elimu ya juu kutoka kaya za walengwa.

Akizungumzia jinsi alivyonufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini bibi mlezi wa Salum, Tabia Gombe anasema amekuwa akipokea Sh. 48,000 mwaka 2015, TASAF ilipoanza kwenye kijiji chao na amepunguziwa hadi kufikia Sh. 32,000 na msaada kusitishwa kipindi cha mlipuko corona.

Gombe anashukuru kwa sababu imemwezesha kusomesha wajukuu zake na kwamba kutokana na hali yake ilivyokuwa mbaya asingeweza labda wangeishia darasa la saba, anaongeza kuwa mjukuu wake Mwajuma yuko kidato cha pili Sekondari ya Mikese na bila TASAF anaamini asingeweza kuisaidia familia yake.

"Pamoja na majukumu ya kusomesha wajukuu, chakula na matibabu nimetumia fedha nilizopewa na mfuko huo kulipa vibarua kunisaidia kulima, kupanda na kuvuna mbaazi kwenye bustani iliyopo nyumbani na hicho ni chakula na familia yangu."

Aidha, anasema fedha iliyobaki ameinunulia mabati 11 na kuezeka nyumba yake ambayo mabati yake yalikuwa yamechakaa.

Anauomba mfuko kuendelea kuwasaidia wahitaji wa kaya maskini kwani bado wanawahitaji kutokana na hali ya maisha kuwa ngumu.

Anashukuru TASAF kwani imewawezesha kula milo miwili hadi mitatu kwa siku tofauti na zamani walikuwa mlo mmoja uliokuwa wa kutafuta ambapo watoto walikuwa wakishindia maembe kwenye msimu huo.

Ofisa malalamiko wa mfuko Dismas Makwinja, anasema, kupitia TASAF serikali ina mpango wa kurejesha pato la wananchi kwa wananchi kupitia mradi wa kunusuru kaya maskini na kwamba wanatarajia kutoa ajira za muda katika kipindi ambacho si msimu wa kilimo wala mavuno vijana waliomaliza elimu ya msingi au sekondari na kushindwa kuendelea na masomo wakifanya kazi kwa saa hadi nne kwa siku watalipwa ujira.

Anawataka vijana kutokata tamaa na kuona umuhimu wa kuwa na moyo wa kujituma kwani mpango huo ukiiva utawasaidia na kuwainua kiuchumi na pia anawashauri wanawake na vijana kuona namna ya kuunda vikundi na kuanzisha biashara ili iwe njia rahisi kwao kupata fedha za vikundi, kuwekeza kwenye biashara mpango ambao utaanzishwa na TASAF hivi karibuni.

Makwinja anasema mpango huo utayasaidia makundi hayo ya wanawake na vijana kuendesha vyema biashara zao na kuwekeza kiuchumi kwa kuwa na utaratibu wa kuweka na kukopa na hivyo kukua kibiashara na kiuchumi na kuzidi kutambua taasisi hiyo kama mkombozi wa jamii na njia sahihi ya kuifanya Tanzania kwa kuingia kwenye uchumi wa kati.



Salum Pandu akimshukuru mhariri Scholastica Mazula baada ya kumkabidhi mchango wa pesa za fomu ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. **PICHA: MWANDISHI WETU**

# Mlipuko COVID-19 ulipotajwa kulipua mimba na ndoa utotoni

**INATOKA UK.11**

na nimeshuhudia wapo wengi. Natoa ushauri kwa wazazi na walezi tuachane na mila za kizamani, tusiozeshe wanafunzi ndoa za utotoni, bali tuwaache watimize ndoto zao," anasema Kabeshi.

Victoria Maro ni Ofisa wa Dawati la Jinsia na Watoto Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga, anasema kwa sasa matukio ya ukatili dhidi ya watoto yameshika kasi zikiwamo ndoa za utotoni, na kubainisha kuna kesi nyingi hivi sasa zinaendelea mahakamani zikiwamo za mimba na ndoa za utotoni.

Anasema dawati hilo kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali na maofisa ustawi jamii na maendeleo wa halmashauri, wameanza kutoa elimu ya kupinga matukio hayo kwa wananchi kwa kufanya mikutano ya hadhara katika maeneo ya vijijini, kutoa elimu juu ya madhara ya kuozesha mwanafunzi na sheria zikoje.

"Tumekuwa tukipokea kesi nyingi sana za ukatili dhidi ya watoto hapa kwenye dawati letu la polisi zikiwamo za ubakaji, mimba, na ndoa za utotoni, na matukio haya yanafanywa na ndugu pamoja na wazazi wa watoto, jambo ambalo tunajihoji labda hawana elimu ya kutosha juu ya madhara ya matukio haya, ndiyo maana tumeanza kutoa elimu," anaongeza.

Katibu wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kupunguza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (Mtakuwwa) mkoani Shinyanga, Tedson Ngware, anasema alama ambayo anataka kuiacha mkoani humo ni kumaliza tatizo la ndoa za utotoni.

Anasema, kwa sasa wanapanga mikakati ya kutunga sheria ndogo, ambazo zitakuwa zikiwabana watendaji wa vijiji na kata kwenye ndoa hizo za utotoni kwa sababu, wanazifahamu kwani wanakaa karibu na wananchi na wanafahamu mipango yote ya harusi, lakini wamekuwa hawatoi taarifa na wakati mwingine wanadaia hushiriki hata kwenye sherehe za ndoa hizo. "Napanga kitu kingine, kuzuia wanafunzi kwenda kwenye magulio na minada, sehemu ambazo ndiko wanadanganywa na kupata wanaume wa kuwarubuni na kuamua kuwaoa ndoa za utotoni na kisha kuwaachisha masomo," anasema Ngware.

"Katika kipindi cha likizo ya corona ndani ya miezi mitatu wanafunzi 101, walipewa ujauzito na kuacha masomo mkoani Shinyanga na hizo ni mimba ambazo zilitolewa taarifa, lakini bado hatujafanya utafiti na kujua hali halisi kwa kupata idadi ya wanafunzi wote walioolewa ndoa za utotoni," anaongeza.

Aidha, anatoa ushauri kwa mahakama kutenga mahakimu ambao watashughulikia kesi za ukatili dhidi ya watoto, jambo ambalo litasaidia kwa kiasi kikubwa kuharakisha usikilizwaji wa mashauri ya kesi hizo na kutolewa hukumu, ili kuzuia kuchelewa mashauri hayo na watuhumiwa kuachiwa huru kwa maelezo mbalimbali.

ELIMU

NA FAUSTINE FELICIANE

# Kwa taarifa, ukame ni chanzo cha maradhi kama ilivyo mvua

PENGINE wengi huamini kuwa mlipuko wa magonjwa hutokea kipindi cha mvua nyingi au mafuriko kwa vile uchafu huchanganyika na maji yanayotiririka na kusababisha vimelea vingi vya maradhi kusambaa. Aidha, mafuriko hubomoa miundombinu hasa vyoo, makaro na mitaro na kusambaza taka za vyooni.

Hata hivyo, pamoja na kuamini kipindi cha mvua nyingi kuwapo na mlipuko wa maradhi Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), inasema wakati wa ukame unaoambatana na uhaba wa majisafi na salama, magonjwa nayo huibuka.

TMA hivi karibuni inatoa utabiri wa msimu wa vuli kwa mikoa ile inayopata mvua mara mbili kwa mwaka na kunaonyesha kuwapo kwa ukame kwa baadhi ya maeneo hayo.

Mikoa hiyo inayopata mvua za vuli na masika ni Mwanza, Geita, Shinyanga, Simiyu, Mara na Kagera. Mingine ni Kilimanjaro, Tanga, Manyara na Arusha

Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agness Kijazi, anasema kuwapo kwa mvua za chini ya wastani katika maeneo hayo kunaweza kukasababisha athari katika sekta mbalimbali zikiwamo kilimo, mifugo na afya.

"Katika sekta ya afya magonjwa ya mlipuko ambayo tumezoea kuyaona kipindi cha mvua nyingi tunatarajia yatakuwapo kwenye msimu huu wa upungufu wa mvua kwa mikoa ambayo inapata mvua mara mbili kwa mwaka, hii ni kwa sababu katika kipindi hicho cha mvua za chini ya wastani kutakuwa na ukosefu wa maji safi na salama," anasema Dk. Kijazi.

Kwa tahadhari hii ambayo imetolewa na TMA, ni vyema sasa kwa mamlaka zinahusika kwenye sekta ya afya kuanza kuchukua hatua mapema ya kukabiliana na hali hiyo iliyotajwa kama itatokea hivyo.

Lakini, pia kwa wananchi mmoja mmoja katika ngazi ya familia wameaswa kuhakikisha hakuna mazalia ya wadudu wanaosababisha magonjwa kwa kuyaharibu na kuimarisha usafi.

Sekta ya afya ni eneo moja tu kati ya maeneo mengi ambayo TMA imesema ni muhimu kuwa makini kutokana na kuguswa moja kwa moja na athari za ukame unaotarajiwa katika kipindi cha miezi michache ijayo.

Ni wazi kuwa ujumbe wa TMA unazifikia mamlaka za miji, nishati na madini, maji, usafirishaji, utalii na wanyama pori pamoja na kilimo na uvuvi.

### ATHARI KILIMO

Hii ni sekta muhimu na nyeti kwa sababu inagusa wakulima moja kwa moja, TMA inatoa tahadhari juu ya suala la kilimo linavyoweza kuathirika kutokana na ukame unaotarajiwa.

Mkurugenzi Mkuu Kijazi anawataka wasimamizi wa sekta hii kutoa elimu na ushauri wa namna ya kupanda mazao himilivu ukame ili kuweza kupambana na madhara yatakayoweza kutokea kutokana na ukosefu wa mvua.

"Hapa tunetegemea kuwapo kwa upungufu wa unyevunyevu katika udongo kwenye maeneo mengi, hali hii itakayochangia kwa kiasi kikubwa ukuaji hafifu wa mazao na hivyo uzalishaji kupungua pia miongoni mwa wakulima wanashauriwa kupanda mazao yanayoweza kukomaa kwa muda mfupi au yale yanayovumilia ukame," anasema Dk. Kijazi.

"Hata hivyo hapa kwenye sekta ya kilimo ndipo maofisa ugani wanapaswa kufanya kazi zao kwa karibu na wakulima kwa ushauri bora wa ina ya mazao wanayotakiwa kulima."

### MIFUGO NA UVUVI

Mikoa ya Kanda ya Ziwa ni mikoa inayosifika kwa uvuvi kutokana na kuwapo kwa Ziwa Victoria, lakini ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo na wanyama wengine wakiwamo punda.

Kwa mujibu wa utabiri wa TMA inaonyesha kuwa sehemu hizo ni miongoni mwa mikoa itakayoathirika na ukame unaotarajiwa kuendelea hadi mwanzoni mwaka.

Ni vyema wafugaji na wakulima kuanza kujipanga kukabili uhaba wa mazao ya ziwani kama samaki, lakini malisho ya mifugo yao itakuwa na changamoto kutokana na ukosefu wa mvua.

Ni wazi bila kujipanga mapema na kuchukua hatua, kuna uwezekano wa migogoro ya wafugaji na wakulima kuzuka kutokana na kugombania malisho na maeneo ya kulima.

"TMA inashauri kwa wafugaji na wavuvi kutumia utabiri wa hali ya hewa na kufuata ushauri wa maofisa ugani ni kipindi ambacho kwa wavuvi wataona kupungua kwa samaki lakini pia mifugo kukosa malisho," anasema Dk. Kijazi.

### TAHADHARI WANYAMAPORI

Lakini, sekta ya utalii na wanyamapori nayo inapaswa kuchukua hatua stahiki kukabiliana na hali ya ukame kwa sababu kuu mbili.

Kwanza kwa upande wa wanyamapori kutakuwa na uvamizi wa makazi ya watu katika kutafuta chakula na maji kutokana na ukame mbugani, hivyo ni vyema kwa mamlaka husika kuanza kuchukua hatua hili kuzuia madhara makubwa yanayoweza kutokea, anasema Dk. Kijazi.

Anaeleza kuwa kuna uwezekano mkubwa wa wanyama kupishana na wanadamu vijijini, "Wapo wale wanyama wanaofugwa wanaweza wakasambaa huku wale wa maporini wakivamia makazi ya watu pembezoni na maeneo ya hifadhi kutafuta chakula, lakini pia kipindi hiki kina hatari ya kusambaa magonjwa ya wanyamapori, ni vyema kwa wahusika kwenye sekta hii kuchukua hatua za kupambana na hali hii kama itajitokeza," anasema Mkurugenzi wa TMA.



Licha ya kusababisha mazalia ya wadudu na vimelea na kuleta magonjwa, ukame pia huathiri sekta ya mifugo kwa kuwakatili wanyama chakula kutokana na nyasi kukauka. **PICHA: MTANDAO.**

> "TMA inashauri kwa wafugaji na wavuvi kutumia utabiri wa hali ya hewa na kufuata ushauri wa maofisa ugani ni kipindi ambacho kwa wavuvi wataona kupungua kwa samaki lakini pia mifugo kukosa malisho," anasema Dk. Kijazi.

### NEEMA USAFIRISHAJI

Sekta pekee ambayo inaweza ikawa katika hali nzuri na salama kutokana na ukame huo ni usafirishaji, kipindi hiki cha ukame hakutarajiwi kuwapo kwa uharibifu mkubwa wa miundombinu kama inavyotokea wakati wa mvua nyingi na mafuriko, anasema Dk. Kijazi.

Yapo maeneo ambayo kwa hakika yamekuwa korofi kipindi cha mvua, yapo maeneo ambayo kunapokuwapo kwa mvua ndogo hujaa maji na kuwa kero kwa wananchi na watumiaji wa maeneo hayo.

Hiki ni kipindi ambacho mamlaka za miji na majiji kutumia nafasi hiyo kujenga na kukarabati maeneo hayo korofi hususani yale yanayokuwa na shida wakati wa mafuriko.

Anawakumbusha kuwa ni wakati wa kuimarisha mitaro ya kupitisha maji kandokando ya barabara kubwa, lakini kujenga madaraja maeneo ambayo yamekuwa korofi kutokana na maji kutuama.

### MIPANGO YA SERIKALI

Kamati ya Maafa iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo yenye jukumu la kuratibu na kutoa maelekezo kwa kamati za mkoa namna ya kupambana na kujikinga na maafa yanayotokana na mafuriko au ukame.

Msemaji wa Kamati ya Maafa, Ibrahimu Hashim, anasema kamati za maafa zikiwa chini ya makatibu tawala zina kazi ya kufuatilia athari zote ambazo zinaweza kutokea wakati wa maafa.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Profesa Faustine Kamuzora, anasema: "Tutaitisha kikao baada ya kupata taarifa rasmi ya kuwapo kwa ukame, kikao kinaangalia namna gani tutapambana na hali hiyo, tunasubiri taarifa rasmi."

Ni vyema kwa makatibu wote tawala wa mikoa ambao ndiyo wenyeviti wa kamati za maafa kuanza kuchukua hatua ya namna gani kupambana na hali inayoweza kujitokeza kutokana na kukosekana kwa mvua.

Anasema katika kipindi cha mvua za vuli kitachodumu kuanzia Septemba mpaka Januari mwakani.

ELIMU

NA SABATO KASIKA

# Wanafunzi sasa waingia vitani kupigana mimba, ndoa utotoni

KATIKA jitihada za kuwanusuru wasichana na rushwa ya ngono kwenye elimu na kazi, mimba pamoja na ndoa za utotoni, wanafunzi wa ngazi mbalimbali wametangaza kubeba jukumu la kupambana na kutokomeza maadui hao.

Wanafunzi walijitosa katika vita hiyo ni wa kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu, kwa vile ndiyo waathirika wakubwa wa vitendo hivyo, ambavyo wanakumbana navyo kuanzia ndani ya familia, jamii hadi shuleni.

Wanasema hayo kwenye mkutano wa uchaguzi wa viongozi wa Jukwaa la Vijana Wanaharakati wa Haki za Vijana Wanawake (YFF), jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki.

Wanavyuo hao na wenzao kutoka shule za msingi na sekondari mbalimbali nchini, wanasema, wana ajenda nyingi zinazowahusu, lakini haziwezi kutimia iwapo kuna tatizo la mimba, ndoa za utotoni na rushwa ya ngono zinazowakabili.

Wanamuomba mwenyekiti waliyemchagua kusimamia ajenda ya kumaliza changamoto hizi ili watoto wa kike waweze kutumiza lengo na ndoto zao katika elimu badala ya kukumbana na vikwazo hivyo.



Wanachama wa Jukwaa la Vijana Wanaharakati wa Haki za Vijana Wanawake wakiwa kwenye mkutano wa uchaguzi wa viongozi wao. **PICHA: SABATO KASIKA**

### MADAI YAO

Happiness Mbise ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ardhi, anasema, viongozi wao wakutane na majukwaa mengine na kuhamasisha vita dhidi ya mimba na ndoa za utotoni na kutoa elimu ya afya ya uzazi shuleni ili kupunguza tatizo hilo kama si kulimaliza kabisa.

Anasema njia pekee ni viongozi wa jukwaa hilo, kuandaa utaratibu wa mikutano ya kuhamasisha jambo hilo kwa kutembelea shule mbalimbali nchini na hata kufanya matamasha kwa ajili kupinga mimba na ndoa za utotoni.

"Suala hili tusiachie serikali na wadau wengine, bali sisi wenyewe tuwe mstari wa mbele kulipinga, hivyo viongozi mlione hilo na kuliweka mbele zaidi ingawa vijana wa kike tuna ajenda nyingi, lakini hilo ni muhimu," anasema Mbise.

Hanifa Pinto, mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anasema, rushwa ya ngono ipo katika vyuo vikuu na sehemu za ajira akiwashauri wasichana kuwa makini.

"Tumezungukwa na mtego huo kuanzia vyuoni na hata kwenye ajira, hivyo jukwaa letu liwe mstari wa mbele kukomesha na kupiga vita tatizo hili ambalo linamdhalilisha mtoto wa kike," anasema Hanifa.

Kwa upande wake mwanafunzi mwingine wa chuo hicho, Zawadi Kondo, anasema, umefika wakati sasa wanafunzi ambao wako miaka ya mbele kuwasaidia wapya wanaojiunga na vyuo, kuepuka mtego huo.

"Sisi wa zamani ambao tupo vyuoni, hatuna budi kuwafundisha wenzetu wapya ili wajue mitego yote ya rushwa ya ngono na jinsi ya kuiepuka, kuliko kuwaacha wanajiendea tu," anasema Zawadi.

### KICHOCHANGIA

Inaelezwa kuwa kuna sababu mbalimbali zinazochangia mtoto wa kike kupata changamoto mimba na ndoa za utotoni, ikiwamo ukosefu wa elimu na taarifa sahihi za afya ya uzazi na hali duni ya maisha.

Haya yanasemwa katika mkutano huo na Salha Azaz, Mkurugenzi wa Asasi ya kiraia ya Binti Salha Foundation, inayotetea haki, elimu na afya mtoto na za vijana wa kike.

"Hali hiyo inasababisha watoto wa kike kukosa mahitaji mbalimbali ya shule na kuingia katika vishawishi vinachangia kuwafanya wapate mimba za utotoni na kuozeshwa ndoa za utotoni na kupoteza malengo yao," anasema Salha.

Anawataka viongozi wa jukwaa hilo, kushiriki kikamilifu katika vita na utoaji wa elimu ya kutosha kwenye jamii, ili ibadilike na kumlinda na kumsaidia mtoto wa kike ili atimize ndoto zake kwenye elimu.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Agenda ya Vijana Tanzania, Rogers Fungo, anawataka vijana hao kufanya ushawishi bila kuchoka, ili hatimaye jamii itambue kilio chao hasa kwenye mambo yanayowahusu.

Anasema, vijana wana mambo mengi yanayowahusu, likiwamo suala la uongozi, ajira na mambo mengine muhimu na kwamba wakiwa kitu kimoja itakuwa rahisi kumaliza hata hayo matatizo ya mimba na rushwa ya ngono.

### WITO WA WALEZI

Jukwaa hilo linalolelewa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ambapo Ofisa Progamu wa Idara Uchechemuzi na Ujenzi wa Nguzo za Pamoja, Florah Ndaba, anawataka vijana wote nchi kuwa sehemu ya jukwaa hilo.

"Ninawahamasisha kutoka ngazi mbalimbali ya jamii, shule na vyuo kutamani kuwa sehemu ya YFF, kwani jukwaa la wazi na linakaribisha vijana wanawake Tanzania," anasema Florah.

Aidha, ofisa huyo anazitaka asasi za vijana kushirikiana na wajumbe wa jukwaa hilo katika mikutano mbalimbali ya kimaamuzi ikiwamo ya kitaifa na kimataifa ili kuunganisha nguvu kumtetea kijana wa kike.

"Jukwaa hili limeanzishwa kama sehemu ya kuendeleza ajenda ya ukombozi wa mwanamke kimapinduzi kupitia vijana wa kuanzia miaka 15 hadi 30 kama ilivyo dira ya TGNP kuhakikisha kuna usawa wa kijinsia," anasema.

Florah anafafanua kuwa uongozi wa YFF unalenga kujenga nguvu ya pamoja na uelewa zaidi wa masuala ya kijinsia, na kwamba vijana wa kike wana wajibu wa kushirikiana kusukuma ajenda yao kwa pamoja.

### MIMBA, RUSHWA

Kumekuwa na tuhuma kuwa baadhi ya wanachuo wa kike wanalazimika kufanya ngono na baadhi ya walimu na wahadhiri ili kufaulu masomo yao.

Tuhuma hizo zinawagusa baadhi ya wahadhiri, kuwa wamekuwa wakilaumiwa kwa kuwanyanyasa kijinsia wanafunzi wa kike kwa kuwaomba rushwa ya ngono au kuwajengea mazingira ya kuwataka kimapenzi.

Kwa mfano, Juni mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, anaitaka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani humo kushirikiana na uongozi wa vyuo vikuu, elimu ya juu na klabu za kupinga ngono vyuoni kuhakikisha wanakomesha vitendo vya rushwa ya ngono vyuoni.

Anatoa agizo hilo wakati akifungua mafunzo ya siku moja ya kupambana na rushwa ya ngono vyuoni kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na elimu ya juu mkoani humo, huku ikibainishwa kuwa rushwa ya ngono vyuoni ina madhara makubwa kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

Anasema, rushwa ya ngono vyuoni inasababisha kuporomoka kwa elimu na sifa ya taaluma ya vyuo vikuu na elimu ya juu, kupatikana kwa wasomi wenye uwezo duni wasio na sifa stahiki, wasomi kupata vyeti wasivyostahili.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) inaitaja mikoa inayoongoza kwa kiwango kikubwa cha mimba za utotoni kuwa ni mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa asilimia 59, Tabora 58, Mara 55, Dodoma 51 na Lindi ni asilimia 48.

Mingine ni Mbeya asilimia 45, Singida 42, wakati Rukwa ina asilimia 40, Ruvuma 39, Tanga 29, Arusha 27, Kilimanjaro 27, Kigoma asilimia 20, Dar es Salaam asilimia 19 na Iringa ni asilimia nane.

Hiyo ni taarifa ya Juni mwaka huu inayotolewa na Ofisa Habari, Albano Midelo, huku akifafanua kuwa Dodoma inatajwa kuwa miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa mimba na ndoa za utotoni, ambapo asilimia 51 ya wasichana wenye miaka kati ya 20 hadi 22 wameolewa kabla ya kufikia miaka 18.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Binti Salha Foundation, Salha Aziz, akizungumza kwenye mkutano wa uchaguzi wa viongozi wa jukwaa hilo. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Youth Vision Association (TYUA), Yusuph Bwango na Mwenyekiti wa Agenda ya Vijana Tanzania, Rogers Fungo. **PICHA: SABATO KASIKA**





# Serikali yaipa TEMESA maagizo 7

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mkuu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Elius Mwakalinga, ametoa maagizo saba kwa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), ikiwamo kufanya ukarabati wa vivuko vyote vyenye hitilafu.

Mwakalinga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dodoma, alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa Baraza la Wafanyakazi wa TEMESA.

Alisema, vivuko vingi katika maeneo mbalimbali ya nchi vimeripotiwa kuwa na hitilafu, lakini hadi sasa TEMESA hawajafanyia ukarabati kwa wakati.

"Mmekaa kimya bila kuvifanyia ukarabati lazima muwe makini hamtakiwi kucheza na maisha ya watu, lazima mvifanyie kazi kwa wakati kabla lolote kutokea," alisema Mwakalinga.

Alieleza kivuko cha Pangani mkoani Tanga na cha Mv Misungwi mkoani Mwanza vimeripotiwa kuwa na hitilafu kwa muda sasa, lakini hakuna hatua zilizochukuliwa na TEMESA.

**Mifumo hii ni ile ambayo sisi pia tutaweza kuona kila tunachokifanya kama kuna udanganyifu tunaona kama ilivyo hivi sasa kwenye mifumo tuliyoifunga kwenye mizani ya barabarani.**

Pia, alisema kuwa kabla ya kuondoka katika nafasi hiyo TEMESA, wahakikishe kuwa cherezo ya kutengeneza vivuko pamoja na karakana kwa ajili ya ukarabati vinakamilika.

"Lazima TEMESA, muwe na cherezo yenu badala ya kuendelea kutumia zile za watu binafsi ambao ukiwakuta wana kazi zao za kutengeneza meli kutoka nchi zingine kama vile Kenya, lazima kwanza msubiri na wakati huo vivuko vyenu vinasimama kutoa huduma," alisema.

Aidha, aliagiza TEMESA kuhakikisha kuwa wanafunga mifumo ya ukusanyaji mapato ili kudhibiti upotevu uliopo sasa.

"Kivuko kile cha Kigamboni ni moja kati ya maeneo ambayo yanatengeneza sana fedha ningekuwa mimi ndiyo mtu wa TEMESA, ningehamishia ofisi yangu pale kwani watu wanakata hadi tiketi za ziada, lakini kama mtafunga mifumo mtapata mapato mengi," alisema Mwakalinga.

Alisema pia serikali ipo katika hatua za kuwa na mifumo ya ukusanyaji wa mapato katika karakana na vivuko vyote kwa kufunga mifumo ya kielektroniki ya kukusanya mapato ili kuondoa ubadhirifu uliopo sasa.

"Mifumo hii ni ile ambayo sisi pia tutaweza kuona kila tunachokifanya kama kuna udanganyifu tunaona kama ilivyo hivi sasa kwenye mifumo tuliyoifunga kwenye mizani ya barabarani," alieleza.

Aidha, aliutaka uongozi wa baraza hilo kuhakikisha kuwa inakuwa mstari wa mbele kupiga vita vitendo vya rushwa, ambavyo vimekuwa vikifanywa na baadhi ya watumishi.

Alisema, hivi sasa pamekuwapo na vitendo vya udanganyifu hasa katika ununuzi wa vipuli vya magari pamoja na mitambo mbalimbali, ambavyo havina ubora kwa gharama za juu tofauti na bei halisi.

Aidha, alilitaka baraza hilo kuhakikisha kuwa linajadili kwa pamoja masuala mbalimbali ikiwemo malalamiko ya watumishi ambao baadhi yao wanadai kutolipwa kwa wakati mishahara yao kwa zaidi ya miezi sita sasa.

"Lazima mjadili suala hilo kwa pamoja ili mtoke na maazimio kwanini wafanyakazi wengine walipwe mishahara kwa wakati na wengine wasilipwe kwa zaidi ya miezi sita au wengine wanapatiwa mikataba ya miezi mitatu na wengine mwaka mmoja, hapatakiwi kuwapo na 'substandard'," alifafanua. Mwakalinga

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Wakala huo, Japhet Maselle, alisema katika mwaka wa fedha 2019/20 wametekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa maegesho, ununuzi wa vivuko pamoja na miundombinu yake ambapo miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji wake.

Kuhusu ujenzi wa vivuko vipya, alisema TEMESA, imekamilisha ujenzi wa kivuko cha MV Ilemela, ambacho tayari kinatoa huduma.

Mwenyekiti huyo, alisema katika mwaka wa fedha 2020/21 wanatarajia kukarabati vivuko vya Mv Tegemeo, Mv Musoma, Mv Nyerere na Mv Kilombero II.

"Wakala unaendelea na ununuzi wa boti tano ambazo zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi na mikataba imeishasainiwa," alisema.

## TAMISEMI yataka utunzaji vifaa, mashine hospitalini

**Na Paul Mabeja,** KONGWA

WAGANGA wakuu wa mikoa na halmashauri nchini wameagizwa kuhakikisha mashine na vifaa vyote vilivyopelekwa katika maeneo yao vinafanya kazi ipasavyo, ili kuboresha utoaji wa huduma za afya.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Afya, Dk. Dorothy Gwajima, baada ya kubaini mashine ya kufulia nguo za hospitali katika Kituo cha Afya Mlali, Wilaya ya Kongwa haifanyi kazi tangu imepelekwa mwaka jana.

Akiwa katika ziara yake Kijiji cha Mlali ya kukagua miundombinu bora ya vyoo kwenye Kaya za Kongwa inayotekeleza mpango maalumu wa usafi wa mazingira (WASH), Dk. Gwajima alitoa siku saba kwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kuhakikisha mashine hiyo inaanza kufanya kazi.

"Natoa siku saba mashine hii isipofanya kazi nakuja kuihamisha na kuipeleka katika vituo vingine vilivyojengwa ili ikatoe huduma stahiki badala ya vituo hivyo nao kuanza mpango wa kununua nyingine wakati hii ipo hamtumii wakati mlisema mnahitaji na serikali ikaleta," alisema.

Aidha, aliitaka timu ya afya Wilaya ya Kongwa (CHMT) kuacha uzembe na kutekeleza majukumu yao kwa kasi ili kuhakikisha wananchi wanahudumiwa na kupatiwa huduma bora za afya katika maeneo yao.

Alitoa kwa kamati za usimamizi wa vituo vya afya kuhakikisha wanafanya ufuatiliaji na usimamizi wa karibu wa masuala yasiyo ya kitaalamu yanayohusu uongozi na matumizi sahihi ya rasilimali ili kuhakikisha huduma zilizokusudiwa kila kitengo zinatolewa.

Kwa upande wake, Kaimu Mganga Mkuu wa Kituo cha Afya Mlali, Dk. Alanus Bagambabyaki, aliahidi kuhakikisha anazingatia maelekezo ya kiongozi huyo.



Mwenyekiti wa kikundi cha Tusumuke cha jijini Dodoma, Christopher Dioniz (wa pili kulia), akiwa na Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Nzuguni, Asha Chogohe (kulia), wakitoa msaada wa vyakula pamoja na vitu mbalimbali kwa wazee wa kaya maskini wa kata hiyo, hivi karibuni. **PICHA: PAUL MABEJA**

## Shirika lanoa wanafunzi kutimiza malengo

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

SHIRIKA la Jukwaa la Utu wa Mtoto (CDF) linalotekeleza Mradi wa Haki ya Binti wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma, limetoa mafunzo ya uongozi na stadi za maisha kwa wanafunzi wa shule za sekondari na msingi ili kuwasaidia kutimiza malengo.

Mafunzo hayo yametolewa kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari Pwaga, Kibakwe, Kimagai na Shule za Msingi ni Lupeta na Ibumila kwa ufadhili wa Comic Relief.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mafunzo hayo, Meneja Utekelezaji wa Miradi ya CDF, Evance Rwamuhuru, alisema mafunzo hayo yamelenga mambo manne ikiwa ni pamoja na kujitambua katika malengo waliojiwekea.

Malengo mengine ni kuwajenga katika stadi za maisha, kuwajengea uelewa katika masuala ya afya ya uzazi na kuwajengea uwezo katika masuala ya uogozi.

"Mafunzo haya yamelenga kuwajenga wasichana pamoja na wavulana wa shule za msingi na sekondari ambao wako 22, tumewafundisha wao kama waelimisha rika kwa maana ya kwamba wao wajifunze na waende kuwafundisha wenzao katika jamii walizotoka," alisema Evance

Aliongeza: "Kupitia mafunzo haya watajiwekea malengo ya sasa na ya baadaye wanapita katika mchakato mzima wa kujua kuwa wao ni kina nani, wana ndoto gani za maisha lakini vikwazo gani watakabiliana navyo."

Pia, alisema matarajio ya mradi huo ni kuhakikisha kuwa watoto wa kike wanafahamu haki zao na wajisimamie kwani hawataraji kuona watoto wa kike wanashindwa kuendelea na masomo yao kwasababu ya kupata ujauzito.

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Pwaga, Lidya Joseph, alisema amejifunza namna ya kujitambua, katika mafunzo hayo kujua mwanafunzi shuleni amekwenda kufanya nini.

"Nimejifunza namna ya kuweka malengo katika masomo yangu, lakini kitu kingine nimejifunza juu ya hedhi salama, hivyo unapokuwa katika hedhi ni vitu gani msichana ufanye, ikiwemo pia kutojichafua kwani hedhi sio ugonjwa lakini pia tumejifunza stadi za maisha, hii itanisaidia sana katika masomo yangu na hata katika maisha," alisema.

Naye Deborah Enock, mwanafunzi wa Shule ya Msingi Ibumila, alisema amejifunza namna ya kujiwekea malengo.



# Walia DC kuzuia ujenzi wa shule

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WAKAZI wa Kijiji cha Yala, Kata ya Itamboleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wamemlalamikia Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, kwa kuwazuia kuendelea na ujenzi wa Shule ya Msingi Mwashikamile kwa maelezo iko ndani ya shamba la mwekezaji wa Kapunga Rice Project.

Wamemwomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, kuingilia kati suala hilo kwa madai kuwa linazidi kupanua mgogoro kati ya wananchi na mwekezaji na kwamba endapo waziri hatalishughulikia watafika mpaka kwa Rais John Magufuli.

Wananchi hao waliambia Nipashe kuwa awali mgogoro huo haukuwahi kuwagusa na badala yake ulikuwa unakigusa kijiji cha Kapunga pekee.

Mzee Nelson Mwashikamile, alisema yeye alikuwapo kijijini hapo wakati mwekezaji wa shamba la Kapunga anabinafsishiwa shamba hilo ambalo lilikuwa linamilikiwa na Shirika la Taifa la Kilimo na Chakula (NAFCO), na kwamba mipaka ya shamba hilo inaeleweka.

**Kabla ya kuanza ujenzi wa shule hiyo, eneo hilo lilipimwa na serikali na kubaini kuwa lina ekari saba na kwamba hata wakati wa ujenzi wa miundombinu ya awali, serikali ilitoa mchango wake.**

"Hii shule tulianza kuijenga miaka saba iliyopita na sasa hivi imefika darasa la sita, hatukuwahi kuzuiliwa kujenga toka mwanzo na ndiyo maana hata halmashauri ilileta fedha hapa za kujenga choo, sasa tunashangaa Mkuu wa Wilaya kuja kutuzuia tusiendelee kujenga," alisema Mwashikamile.

Alisema awali walikuwa wanaporwa mashamba pekee, lakini kwa sasa hali imekuwa mbaya kwa kuanza kuporwa mpaka taasisi za umma ikiwamo shule hiyo.

Naye Manyanya Matabe, mkazi wa kijiji hicho, alisema mwezi Mei, 2019, Rais Magufuli alipokuwa ziarani wilayani humo, aliagiza shamba lenye ukubwa wa hekta 4,600 zirejeshwe kwa wananchi na apelekewe orodha ya waliopewa.

Alisema maelezo hayo ya rais yaliwapa matumaini makubwa, lakini cha ajabu maeneo yaliyokuwa mashamba ya wananchi na makazi yameanza kuchukuliwa tena na kupelekwa kwa mwekezaji hali ambayo inawachanganya tena.

"Kinachoendelea sasa hivi ni kwamba agizo la Rais halijatekelezwa, lakini maeneo ya wananchi ambayo walikuwa wanalima tangu miaka 1960 yanapelekwa kwa mwekezaji, sasa tunashindwa kuelewa kwamba kauli ya rais haikueleweka au kuna wasaidizi wake wanaamua kuitumia vibaya?" Alihoji Matabe.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Kata ya Itamboleo, Mohamed Kakwambi, alisema tatizo hilo linakiletea chama chake matatizo na wananchi hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu.

Alisema wananchi wanaanza kukosa imani na chama hicho wakidai kuwa kimeshindwa kuwasaidia kutatua migogoro ya ardhi ambayo inawasumbua kwa muda mrefu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule ya Msingi Mwashikamile, Emmanuel Mkatasa, alisema shule hiyo ilianza kujengwa mwaka 2014 na kwamba mpaka sasa ina wanafunzi 280 kuanzia darasa la kwanza mpaka la sita, lakini lina vyumba vinne pekee ambavyo vimekamilika na vinatumika.

Alisema kabla ya kuanza ujenzi wa shule hiyo, eneo hilo lilipimwa na serikali na kubaini kuwa lina ekari saba na kwamba hata wakati wa ujenzi wa miundombinu ya awali, serikali ilitoa mchango wake.

Mkuu wa Wilaya, Mfune, alikiri kuzuia shule hiyo kuendelea kujengwa kwa maelezo kuwa eneo hilo lipo kwenye mipaka ya ramani ya shamba la mwekezaji na akasisitiza kuwa pamoja na malalamiko ya wananchi, lakini katazo lake liko pale pale.

Alisema wanaendelea kulishughulikia jamba hilo na wataruhusu ujenzi kuendelea ama kusitishwa kabisa baada ya taratibu zingine kukamilika na kwamba katazo lake ni la muda.

Shule ya Msingi Mwashikamile ni ya pili kudaiwa kuwa iko ndani ya shamba la mwekezaji wa Kapunga Rice Project ambapo mwaka 2011, shule hiyo ilivunjwa kwa madai kuwa ilikuwa ndani ya shamba hilo.



Mtafiti wa matunda kutoka Taasisi ya Utafiti na Kilimo (TARI), kituo cha Uyole, Daud Mbongo (kulia), akifafanua jambo kwa Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba (kushoto), kuhusu aina mbalimbali za mbegu za parachichi zilizobuniwa na kituo hicho, mkoani Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Aitaka TARI kuainisha protini kwenye mikunde

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, ameitaka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole jijini Mbeya kuainisha makundi ya vyakula aina ya mikunde, kiwango cha protini kinachopatikana ili kuwasaidia Watanzania kupunguza gharama za matumizi ya nyama.

Mgumba alitoa maelekezo hayo juzi alipotembelea kituo hicho kwa lengo la kuangalia shughuli za utafiti zinazoendelea kufanyika.

Alisema kwa mujibu wa taarifa za wataalamu, mimea aina ya mikunde ina kiwango kikubwa cha madini ya protini hivyo wananchi wahamasishwe kutumia zaidi kuliko nyama.

"Kiwango kinachopatikana kwenye mimea aina ya mikunde ikiwamo, mbaazi ni kikubwa sana kuliko kinachopatikana kwenye mayai, maziwa au nyama hivyo ni vyema wakulima na wananchi wakahamasishwa kutumia na TARI mna jukumu la kuainisha kila mmea aina ya kiwango kinachopatikana," alisema Mgumba.

Pia aliitaka TARI kufanya utafiti wa masoko ya kuwashauri wakulima ni aina gani ya mbegu, eneo na faida watakayoipata kabla ya kuanza shughuli ya kilimo.

Mkurugenzi wa Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema watayafanyia kazi maelekezo waliyopewa kwa kuhakikisha kila aina ya mmea wa majani ya mikunde wanaweka kiwango cha protini kinachopatikana kabla ya kuwauzia wateja.

Alisema hatua hiyo ni nzuri kwa sababu inalenga kuboresha afya za wananchi sambamba na kuimarisha soko la bidhaa hizo.

# Waendesha bajaji wahimizwa amani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAENDESHA pikipiki za magurudumu matatu (bajaji) jijini Mbeya, wametakiwa kulinda amani hasa katika kipindi hiki cha kampeni za uchaguzi mkuu, badala ya kuwashabikia wanasiasa na kufanya vurugu ambazo zitaathiri hata shughuli zao.

Mlezi wa chama cha waendesha bajaji wa jiji hilo, Ndele Mwaselela, alitoa rai hiyo jana alipofanya mkutano na vijana hao kwa lengo la kujadiliana matatizo yanayowakabili na kutafuta mbinu za kuyatatua ili wafanye shughuli hiyo ya usafirishaji kwa amani.

Aliwataka kuwaepuka wanasiasa wanaowashawishi kufanya vurugu kwa kuwaahidi fedha na kwamba mambo ya siasa wawaachie wanasiasa na wao waendelee kufanya kazi yao kwa kuzingatia sheria mbalimbali zinazowaongoza zikiwamo za usalama barabarani.

Aliwataka waendelee kufuatilia sera za wagombea wa nafasi mbalimbali ili waje wafanye uchaguzi sahihi Oktoba 28, na kwamba yeyote atakayeshindwa kwenye kinyang'anyiro hicho waendelee kushirikiana naye.

"Siasa zinapita, hizi pilika pilika mnazoziona ni za muda mfupi sana, lakini kuna maisha mengine baada ya siasa yataendelea, kwa hiyo nawasihi msikubali kudanganywa na mwanasiasa mkaingia kufanya fujo kwa kuahidiwa 'vipesa' kidogo," alisema Mwaselela.





# Queen Sendiga: Nimegombea urais kutaka usawa kijinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha ADC, Queen Cathbert Sendiga, amesema kuwa usawa wa kijinsia uliopo ndani ya chama chake umemwezesha kugombea nafasi hiyo ya juu.

Akizungumza na Nipashe Mjini Zanzibar, alisema kuwa wanawake wana uwezo mkubwa wa kuwa viongozi katika nafasi za juu, na sio jambo jema kuwaachia wanaume pekee nafasi hizo.

Mgombea huyo aliwataka wanawake kumuunga mkono na kumpigia kura bila ya kuangalia vyama vyao vya siasa ili wanawake kuiongoza serikali ambapo yeye uwezo huo anao.

**Wanawake wana uwezo mkubwa wa kuwa viongozi katika nafasi za juu, na sio jambo jema kuwaachia wanaume pekee nafasi hizo.**

Mgombea huyo alizitaka asasi mbalimbali za utetezi kwa wanawake kumuunga mkono kwa sababu lengo lake ni kuhakikisha sauti za wanawake zinafikiwa na makundi yoye kwa ajili ya kufikisha kilio chao kinachotokana na changamoto zinazowakabili.

"Masikitiko yangu makubwa hakuna taasisi za wanawake zilizojitokeza kuniunga mkono katika kipindi chote tangu nilipochukua fomu za urais na baadaye kupitishwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi," alisema.

Alisema kuwa endapo atapata ridhaa ya kuwa Rais atahakikisha anatengeneza usawa wa kidemokrasia na upatikanaji wa haki za binadamu.

Aidha, mgombea huyo alisema Rais wa Tanzania, John Magufuli katika maeneo aliyofanikiwa ni ujengaji wa miundombinu ya barabara ambayo imesaidia kuiunganisha mikoa ya Tanzania Bara.

"Hivi sasa unaweza kuitembelea mikoa ya Tanzania Bara kwa kutumia miundombinu ya barabara ya lami bila ya matatizo na hivyo kuwawezesha wananchi wa Tanzania kufanya shughuli zao za maendeleo ikiwamo za kiuchumi," alisema.

Alisema chama chake kikifanikiwa kushika madaraka kitajikita zaidi katika kuimarisha kilimo kwa sababu tayari miundombinu ya kuwawezesha wakulima kufikisha mazao yao sokoni tayari ipo.

## TAMWA yataka elimu athari za mimba utotoni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, kimeitaka jamii kusaidia kutoa elimu dhidi ya athari ya mimba na ndoa za umri mdogo ili kuwanusuru watoto na majanga ambayo yanawaathiri kimwili na kisaikolojia.

Akizungumza na waandishi wa habari Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, alisema tatizo hilo litaweza kuondoka endapo nguvu za pamoja zitaungana, wakiwamo viongozi wa dini, wanasiasa na wanaharakati wa masuala ya wanawake kwa kupanga mikakati mahsusi ya kuelimisha jamii athari zinazojitokeza wakati wa kjifungua katika umri mdogo.

"TAMWA Zanzibar hivi karibuni imepokea taarifa za kusikitisha za mtoto aliye chini ya umri wa miaka 15 aliyebakwa na kupata ujauzito na hatimaye kupoteza maisha wakati wa kujifungua," alisema.

Dk. Mzuri alieleza kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa mzazi wa marehemu, tukio hilo limetokea Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba na kwamba alifariki dunia Juni 25, wakati akijifungua.

Alisema TAMWA imefanya uchunguzi kuhusiana na athari za mimba za mapema na kugundua kuna madhara mengi ambayo yanajitokeza katika mimba za mapema ikiwamo kuathirika kimwili na kisaikolojia pamoja na kupoteza maisha, hivyo jitihada za pamoja zinahitajika katika kupambana na janga hilo linalowaathiri watoto ambao ndio taifa la baadaye.

Naye Dk. Kamilia Ali Omar wa kitengo cha wazazi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar, alisema mimba za umri mdogo zinaweza kusababisha ugonjwa wa fistula, saratani ya shingo ya kizazi na magonjwa mengine hujitokeza kutokana na baadhi ya viungo katika mwili havijakomaa.

"Kujifungua chini ya miaka 18 ni kuhatarisha maisha ya mama na mtoto kwa sababu nyonga ya mtoto aliyechini ya miaka 18 haijapea/komaa na kuweza kusukuma mtoto hivyo hupelekea mzazi kuwa katika hali hatarishi ya kupata ugonjwa wa fistula, au mzazi hupoteza maisha au baadhi ya maradhi huenda yakajitokeza kwa baadaye," alisema Dk. Kamailia.



Mgombea urais wa Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Ali Hassan Mwinyi, akimkabidhi zawadi ya ngao mwanafunzi Abdulrahman Abdulla wa Shule ya Biashara Zanzibar, baada ya kupata daraja la kwanza katika ufaulu wa mitihani ya kidato cha sita mwaka huu, akiwa pia mshindi wa kwanza wa jumla Zanzibar, katika hafla ya kuwapongeza wanafunzi waliomaliza kidato cha sita na kufaulu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi awaonyesha fursa ya ajira wahitimu kidato 6

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA wa urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka wanafunzi waliomaliza elimu ya kidato cha sita kuchagua fani nzuri za kusoma katika elimu ya juu, ili kukidhi soko la ajira baada ya kumaliza masomo.

Dk. Mwinyi alisema hayo Mjini Zanzibar wakati akizungumza katika hafla ya kuwapongeza vijana waliomaliza kidato cha sita na kupata ufaulu wa alama ya kwanza, pili na tatu ambao wanasubiri kujiunga na vyuo vikuu mbalimbali nchini.

Mgombea huyo alisema miundombinu imara katika sekta ya elimu ndio njia pekee inayoweza kuzalisha wasomi wazalendo wanaokuwa nguzo imara katika kuimarisha uchumi wa taifa lolote.

Alisema miundombinu hiyo ambayo huenda sambamba na kuwa na mitaala na mazingira bora, takwimu, maslahi ya walimu pamoja na gharama za kuhudmia elimu ni mambo ya msingi yanayotosheleza haja ya kuwa na wasomi wengi ambao ndio nguzo sahihi ya tegemeo la Taifa katika maendeleo.

Alisema iwapo atachaguliwa kuwa rais wa Zanzibar, anakusudia kuupitia upya mfumo wa elimu wa Zanzibar, ili kuwasaidia vijana wanaomaliza elimu ya juu kupata ajira kwa mujibu wa fani walizosomea.

Aliyataja maeneo matano ya elimu ambayo yatafanyiwa marekebisho makubwa na kupitiwa upya ni kuangalia miundombinu ya elimu ikiwamo majengo ya shule kuanzia ya msingi hadi sekondari ili kuwa na hadhi ya juu.

Aidha, alisema anakusudia kuimarisha rasilimali watu ikiwamo maslahi ya walimu ili kujenga uwezo wa juu wa kusomesha wanafunzi na kupata ufaulu wa daraja la juu.

"Katika suala la kuimarisha elimu...nataka kuona maslahi ya walimu yanakuwa bora kwa kupitia upya viwango vya mishahara na taaluma zao kwa ujumla," alisema.

Dk. Mwinyi aliyataja mambo mengine ya msingi ambayo yatapitiwa upya ili kuona kiwango cha elimu kinakuwa bora ni upatikanaji wa vitabu vya kusomea, madawati na kuimarisha maabara za masomo ya sayansi katika shule zote za sekondari.

Alieleza kuwa uchangiaji wa sekta ya elimu itaangaliwa upya ikiwamo bajeti ya Wizara ya Elimu kwa ajili ya kuwapatia wanafunzi mikopo ya juu kulingana na mahitaji yao.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Tabia Mwita, alisema wanafunzi wa shule za sekondari wanaotegemewa kujiunga na vyuo vikuu mbalimbali nchini wapo tayari kuiunga mkono CCM kutokana na sera zake zilizolenga kuwanufaisha vijana.

Kwa upande wake Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, alisema ilani ya CCM ndiyo pekee ambayo imewekeza zaidi katika sekta ya elimu kwa vijana na kuwataja bayana kwamba ndiyo tegemeo la taifa kushika uongozi.

Hafla hiyo ya kuwapongeza wanafunzi wa kidato cha sita waliopata alama ya ufaulu ya daraja la kwanza hadi la tatu iliandaliwa na CCM Zanzibar, utaratibu huo umekua ukifanyika kila mwaka.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**

Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- Kuboresha biashara
- Kulipa kodi ya nyumba
- Kumalizia tenda
- Kulipa matibabu n.k.

Mawasiliano yetu: Dar es salaam **– 0768 928 516. Arusha – 0677 226 960.**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;257/2020

Ombi la SHUKURU DEODATUS CHRISPIN,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu DEODATUS CHRISPIN KASIMBA.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 01/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/09/2020.

Tarehe 4/9/2020

115901802

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI

(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;268/2020

Ombi la TAUSI HASSAN MASENDA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HASSAN SELEMAN MASENDA.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 17/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 14/09/2020.

Tarehe 14/9/2020

HAKIMU
MOROGORO

115901102

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA KILOSA .
S.L.P. 29, KILOSA
06-08-2020

YAH: MAOMBI YA MAOMBI MADOGO NA: 61/2016.
MARIA J. LUPATU.................MLETA MAOMBI

VERSUS

MARINGO MAZURI.........MJIBU MAOMBI
WITO/KUITWA SHAURINI KWA MARINGO MAZURI

Popote Ulipo unaarifiwa Ufike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe 24/09/2020.Wenyewe binafsi au Mwakilishi wako bila kukosa ambapo MAOMBI yamepangwa kutajwa. Endapo hutaudhuria,maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imesainiwa leo **Tarehe 06 Mwezi 08 Mwaka 2020.**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
KILOSA

115901202

---

## OFISI ZA MATANGAZO

**Mikocheni Industial Area,**

**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**

**Mob: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
(DAR ES SALAAM)

MAOMBI YA KUKAZA HUKUMU NA. 86 YA MWAKA 2019

ABDULLAI ABDUL AZIZI.........................MDAI

VERSUS

MBARAKA SHEIKH ALLY SHEIKH............................1. MDAIWA
ALMADINAH SOCIAL SERVICES TRUST.....................2. MDAIWA

KWA: MBARAKA SHEIKH ALLY SHEIKH,
ALMADINAH SOCIAL SERVICES TRUST
DAR ES SALAAM
KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa mleta maombi aliyetajwa hapo juu, amefungua shauri la madai dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati za madai zinapatikana katika Mahakama hii kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria, siku ya tarehe 16/09/2020 saa tatu kamili (3:00) asubuhi mbele ya Mhe. J.E. Fovo, Naibu Msajili kujibu madai hayo dhidi yako. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo. Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama ikithibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama leo tarehe 18 mwezi wa nane 2020.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
KANDA YA DAR ES SALAAM

115901602

---

IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MOSHI DISTRICT REGISTRY
AT MOSHI

BILL OF COST NO.7 OF 2020

EDWARD HELGARD SAM............................DECREE HOLDER

VERSUS

PRIDE TANZANIA
GRM AUCTIONEER & COURT BROKER .........JUDGEMENT DEBTOR

ROBERT KIMARIO
TO:
PRIDE TANZANIA ,
WHERE VER YOU ARE

### NOTICE FOR MENTION

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the High Court Of Tanzania at Moshi on 22nd September, 2020 at 09:am Before Honourable O.H KIGWELE- Deputy Registrar
**WHEREAS:** S ervice on you has been ordered to be published in the NIPASHE newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the document upon which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT:** In default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court , this 14th day of August ,2020

O.H.KINGELE
DEPUTY REGISTRAR

115900302

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI

(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;245/2020

Ombi la NEEMA K.MYUNGA, Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu KALISTUS PIUS MYUNGA.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 29/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 01/09/2020.

HAKIMU
MOROGORO

115901002

---


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**


---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO

TANGAZO LA KUITWA SHAURINI

SHAURI LA MADAI/TARAKA/MIRATHI NAMBA 266/2020

MDAI: ABDULLKARIM SAID NASSORO
DHIDI YA
MDAIWA: SUDI COSMAS CHINGWI

Kwa: SUDI COSMAS CHINGWI

Ombi la Mdai/Muombaji/Msimamizi:
ABDULLKARIM SAID NASSORO

**Madai ya: PESA TSH. 30,000,000/=**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 11 Mwezi 9 Mwaka 2020 saa 2:30 Asubuhi/Alasiri.
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 8 Mwezi wa 9 Mwaka 2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115901702

---

IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MOSHI DISTRICT REGISTRY
AT MOSHI
BILL OF COST NO.7 OF 2020
EDWARD HELGARD SAM............................DECREE HOLDER

VERSUS

PRIDE TANZANIA
GRM AUCTIONEER & COURT BROKER........JUDGEMENT DEBTOR

ROBERT KIMARO
TO:
GRM ACTIONEER & COURT BROKER ,
WHERE VER YOU ARE

### NOTICE FOR MENTION

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the High Court Of Tanzania at Moshi on 22nd September, 2020 at 09:am Before Honourable O.H KIGWELE- Deputy Registrar
**WHEREAS:** S ervice on you has been ordered to be published in the NIPASHE newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the document upon which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT:** In default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court , this 14th day of August ,2020

O.H.KINGELE
DEPUTY REGISTRAR

115900302

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA DODOMA

SHAURI LA ARDHI RUFAA NA.26/2019

ISSA RASHID ALLY.........................................MRUFANI

DHIDI YA

GERALD TEMBA.........................................MRUFANIWA

KWA : GERALD TEMBA
POPOTE PALE ULIPO

**YAH: TAARIFA YA KUSIKILIZWA KWA SHAURI LA ARDHI RUFAA NA 26/2019 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litasikilizwa Mahakama kuu ya Tanzania, kanda ya Dodoma, mbele ya Mhe. Jaji M. M. Siyani, wa Mahakama kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu (3:00) kamili asubuhi siku ya Alhamisi tarehe 24/9/2020.
**HIVYO BASI;** Unatakiwa ufike wewe mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
**NA ENDAPO;** Hutafika wewe mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashugulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au Wakili wako kuwepo;
IMETOLEWA; kwa mkono wangu na mhuri wa mahakama hii leo tarehe 05 Mwezi wa Agosti, 2020.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

115901302

---

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA KINONDONI

SHAURI LA MIRATHI NA.63 YA 2020

USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II

Maombi ya barua ya usimamizi wa mirathi

MODESTER GABRIEL KWENDE..................MAREHEMU

DHIDI YA

GABRIEL KWENDE NDOMBA.................MLETA MAOMBI

Kwa:
GABRIEL KWENDE NDOMBA
DAR ES SALAAM.

TAARIFA YA KAWAIDA
{Kanuni ya 75}

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa waombaji hapo,
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 02 mwezi wa 10 Mwaka 2020.

**Hati hii imetolewa 10 mwezi 09 Mwaka 2020**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

115899502

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SALEH AWADH BALBOU** amepotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri **T 435 AAK** aina ya **CANTER** yenye ingine namba **759848** na chasis namba **0479327** na rb namba **DSM/PHQ/RB/663926/2020.**

115901902

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PATRICK B.J. LYIMO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya MERCEDES BENZ yenye namba za usajili **T 765 AGK.** Chassis no. **WDB1261201A059257,** Egine no.**61795112063476.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOM/RB/2017/2020.**

115901502

---

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II

(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)
Katika Mahakama ya Mwanzo KAWE

Usimamizi wa Mirathi Na. 185/2020

Ombi la NAZARAL MOHAMED NAZARAL kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu MOHAMED NAZARAL SUMAR

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 08/09/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo ya MOHAMED NAZARAL SUMAR
Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 08/09/2020.

SAHIHI YA HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
KAWE

215899702

---

IN THE COURT OF DISTRICT OF DODOMA
AT DODOMA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE
NO.47 OF 2020

In the matter of the Estate of the late HOSEA CHIBITAA CHIMANYI

AND

In the matter of the Application for letters of Administration by STANLEY HOSEA CHIBITAA

### GENERAL CITATION

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letters of Administration) is made to the above named Petitioners.
Objections to the grant should be filed on or before 06th day of OCTOBER, 2020
Date 9th day of SEPTEMBER, 2020.

Resident Magistrate
DODOMA.

115901402

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**GEORGE CHARLES MTONI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0101–0164** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa kupitia AZANIA SEKONDARI mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **URP/RB/488/20.**

115900902

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**Michael B. Madassy** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1967.0064** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2015 katika shule ya Sekondari Changalikwa, Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/KIG/RB/663199/2020**

215899902

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**Justine James** anatangaza kupote kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0313/054** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2011 katika shule ya Sekondari Ikizu na cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S.147/0697** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Pugu, Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochocte cha Polisi. Polisi Taarifa: **TAB/RB/4704/2019**

215899402

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**Stephano Paulo Masatu** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0129/0077** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1990 katika Shule ya Sekondari Mara Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **KJN/B1/VOLXXXII/133**

115900002

---


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Viongozi EU wakutana na China

**BERLIN,** Ujerumani

KANSELA wa Ujerumani, Angela Merkel, maofisa wa ngazi ya juu wa Umoja wa Ulaya pamoja na Rais wa China Xi Jinping jana walifanya mazungumzo ambayo yalijikita katika masuala ya biashara na uwekezaji na kujenga imani ili kushughulikia masuala magumu ya kisiasa yanayotishia kuharibu uhusiano wao.

Merkel, ambaye nchi yake kwa sasa inashikilia urais wa kupokezana wa Umoja wa Ulaya, atajiunga na Rais wa Baraza la Ulaya Charles Michel, Rais wa Halmashauri Kuu ya Ulaya, Ursula von der Leyen na mkuu wa sera ya nje wa umoja huo, Josep Borell kwa mkutano wa video ambao umeanza saa sita kamili kwa majira ya Ulaya.

Mazungumzo kati ya China na Ujerumani, nchi zenye uchumi mkubwa duniani, yataruhusu kutathmini uhusiano wao pamoja na nchi nyengine za Ulaya. Pia mazungumzo hayo yataangazia masuala ya uchumi, mageuzi katika shirika la biashara duniani, mabadiliko ya tabia nchini na janga la virusi vya corona. **DW**

## Maandamano zaidi kumpinga rais Belarus

**MINSK,** Belarus

WABELARUS kwa mara nyingine tena wameandamana dhidi ya kuchaguliwa tena kwa Rais Alexander Lukashenko Jumapili, Septemba 13, 2020.

Maelfu ya watu wanaandamana jijini Minsk na miji mingine nchini Belarus, katika mwendelezo ya maandamano dhidi ya Rais Alexander Lukashenko.

Idadi kubwa ya maofisa wa polisi wameonekana wakijaribu kuwazuaia waandamanaji hao, huku watu zaidi ya 200 wakikamatwa hata kabla ya kuanza kwa maandamano hayo. Maandamano hayo yamekuwa yakishuhudia tangu mwezi uliopita, baada ya uchaguzi mkuu ambao wapinzani wanasema uliibiwa na hivyo wanamtaka Rais Lukashenko ajiuzulu.

Svetlana Tikhanovskaya, mgombea urais aliyedai ushindi dhidi ya Alexander Lukashenko, na ambaye sasa yuko uhamishoni nchini Lithuania, katika video, alipongeza "watu mashujaa wa kweli" ambao wanaendelea na "kupigania uhuru".

# WHO yabaini ongezeko maambukizi ya corona

**NEWYORK,** Marekani

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limesema kuwa limerekodi ongezeko la maambukizi mapya ya virusi vya corona kwa muda wa siku moja na kupata vifo zaidi ya 5,500 na kufanya dunia kuwa na jumla ya vifo 917,417 vilivyotokana na mlipuko huo.

Ongezeko kubwa la maambukizi limeripotiwa kutoka India, Marekani na Brazil. Duniani kote kuna zaidi ya wagonjwa milioni 28 waliothibitika kuwa na virusi vya corona na nusu ya idadi hiyo ni kutoka Marekani. Rekodi ya siku moja ya maambukizi mapya ilikuwa ya Septemba 6, wakati WHO iliporipoti maambukizi mapya 306,857.

Kwa mujibu wa WHO, India imeripoti maambukizi mapya 94,372 siku ya Jumapili na Marekani imeripoti visa 45,523 na Brazil ikiwa ni 43,718. Zaidi ya vifo vipya 1,000 vimerekodiwa Marekani na India wakati Brazil, watu 874 walikufa kutokana na magonjwa yenye uhusiano na Covid-19 ndani ya saa 24.

Wiki iliyopita iliripotiwa karibu milioni mbili ya maambukizi ya virusi vya corona mwezi Agosti, idadi kubwa kurekodiwa tangu mlipuko ulipoanza. Taifa hilo lilishuhudia wastani wa maambukizi 64,000 kwa siku huku 84% ya wastani wa maambukizi yote mwezi Julai kwa mujibu wa takwimu rasmi.

**Jimbo la Victoria limekuwa kitovu cha mlipuko wa maambukizi nchini Australia, huku kukiwa na maambukizi ya 75% na vifo 90% vilivyotokana na virusi vya corona.**

Ongezeko la vifo limefikia 1,000 kila siku tangu mwanzoni mwa mwezi Septemba. Brazil imerekodi zaidi ya wagonjwa milioni nne wa virusi vya corona na kuwa ya tatu duniani kwa kiwango cha juu cha maambukizi. Kuna idadi kubwa ya vifo kutokana na corona maeneo ya Amerika ya Kusini, kwa idadi ya vifo 131,000 mpaka sasa.

Marekani imerekodi karibu robo ya maambukizi ya virusi vya corona duniani ni zaidi ya milioni sita. Ongezeko lilionekana kila siku mwezi Julai, lakini idadi imeshuka tangu wakati huo. Marekani ina idadi kubwa ya vifo vilivyotokana na virusi vya corona, kwa zaidi ya idadi ya vifo 194,000.

Mataifa ya Ulaya, rekodi ya maambukizi bado inaongezeka kila siku huku kukiwa na hofu ya mlipuko mwingine kutokea. Amri ya kutotoka nje imewekwa katika maeneo yenye maambukizi makubwa na watu wametakiwa kuvaa barakoa na kuzingatia kukaa kwa umbali. Mataifa mengine virusi vinaonekana kuibuka tena kama Peru, Israel, Korea Kusini na Australia.

Jumapili, polisi nchini Australia katika Jimbo la Victoria waliwakamata waandamanaji 70 kwa kukiuka sheria ya kukaa nyumbani. Zaidi ya watu 250 walihudhuria katika maandamano hayo katika mji wa Melbourne, walikuwa wanawahamasisha watu kwenye mitandao ya kijamii kuhusu mpango wa nadharia kuhusu mlipuko.

Jimbo la Victoria limekuwa kitovu cha mlipuko wa maambukizi nchini Australia, huku kukiwa na maambukizi ya 75% na vifo 90% vilivyotokana na virusi vya corona.

Kwa sasa Israel imeweka amri mpya ya kuzuia watu kutoka nje kutokana na maambukizi kuongezeka. Makatazo makali yalitolewa Ijumaa katika mwaka mpya wa Wayahudi na sheria hizo zitadumu kwa muda wa wiki tatu, mamlaka imeeleza.

Israel imethibitisha zaidi ya maambukizi 153,000 na vifo1,108 vilivyotokana na Covid-19, kwa mujibu wa takwimu ya Chuo Kikuu cha Johns Hopkins. **BBC**



Waandamanaji wakijitosa mitaani nchini Belarus kuipinga serikali. **PICHA: MTANDAO**

# Mkutano kuijadili Afrika ya Kati waahirishwa

**KINSHASA,** DRC

MKUTANO wa viongozi watano wa nchi za Afrika ya Kati ambao ulitarajiwa kufanyika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Kinshasa, umeahirishwa kwa tarehe isiyojulikana.

DRC imetangaza kuahirishwa kwa mkutano huo uliokuwa umepangwa kufanyika mjini Goma wiki ijayo, kujadiliana kuhusu hali ya usalama katika eneo la maziwa makuu.

Waziri wa Mambo ya Nje, Marie Tumba Nzeza, akitoa tangazo hilo, amesema kuwa mkutano huo utafanyika tarehe nyingine.

Nzeza ameeleza kuwa, hatua ya kuahrishwa kwa mkutano huo imetokana na kuanza kwa Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa utakaoanza Jumanne jijini New York nchini Marekani na viongozi hao wanajiandaa kuhutubia mkutano huo.

Hata hivyo, kabla ya kuahirishwa kwa kikao hicho, Burundi ilikuwa imesema kuwa haitashiriki katika mkutano huo ambao ungewaleta viongozi kutoka Uganda, Rwanda, Angola pamoja na wenyeji Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Duru nyingine zinasema huenda sababu ya kuahirishwa kwa kikao hicho ni viongozi wa Uganda kupendekeza kuwa, kifanyike mjini Lubumbashi ili kumwepusha Rais Yoweri Museveni kupitia katika anga la Rwanda.

Uganda na Rwanda, katika miezi ya hivi karibuni, zimeendelea kuvutana na kusababisha uhusiano baridi kati ya nchi hizo jirani, na DRC pamoja na Angola zimekuwa zikijaribu kutatua mvutano huo.

Mbali na masuala ya usalama, viongozi wa nchi hizo walikuwa wamepanga pia kujadiliana kuhusu uhusiano wa kidiplomasia wa nchi zao na kuanza kurejesha ushirikiano wa kibiashara katika kipindi hiki cha janga la corona. **RFI**

# LAMPARD ASHANGAZWA KAULI YA KLOPP CHELSEA



**LONDON,** England

FRANK Lampard ameishutumu kauli kutoka kwa Jurgen Klopp, juu ya Chelsea kutumia fedha nyingi kwenye usajili, akisema ilikuwa ya "kujifurahisha" wakati Liverpool ina kikosi cha gharama kubwa.

Chelsea imetumia karibia pauni milioni 200 kuwasajili Kai Havertz, Timo Werner, Ben Chilwell, Hakim Ziyech, Malang Sarr na Thiago Silva ikiwa na nia ya kufanya vizuri kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Kwa ulinganisho, Wekundu wa Anfield wamemsajili Kostas Tsimikas pekee kutoka Olympiakos katika dirisha hili kubwa la usajili, huku Klopp akisema Alhamisi iliyopita kwamba, kikosi chake ni "klabu tofauti" na wapinzani wake "kwa kutomiliki nchi au matajiri wa mafuta".

Hata hivyo, Lampard alibainisha kwamba, Liverpool isingeweza kushinda taji lake la kwanza la Ligi Kuu kwa kipindi cha miaka 30 msimu uliopita, kama Klopp asingeungwa mkono kwa kutumia fedha nyingi kuwasajili wachezaji kama Virgil van Dijk, Alisson, Fabinho, Naby Keita na Mohamed Salah kwenye madirisha ya usajili yaliyopita.

Alipoulizwa kuhusu kauli hiyo ya Klopp kuelekea mchezo wake wa jana, Jumatatu wa ufunguzi wa Ligi Kuu kwa 'Blues' hao dhidi ya Brighton and Hove Albion, Lampard aliwaambia waandishi wa habari: "Nimeona anajifurahisha kwa sababu wakati unapozungumzia wamiliki wa klabu, sidhani kama inahusiana hasa kutokana na biashara waliyokuwa wakiifanya.

"Tunazungumzia baadhi ya wamiliki matajiri sana kwenye Ligi Kuu. Kwa habari ya Liverpool, anasahau kama wao wana kikosi cha gharama kubwa.

# Arteta: Willian atakuwa mfano kwa vijana Arsenal

**LONDON,** England

MIKEL Arteta anaamini, Willian atathibitisha kuwa ni mfano kwa wachezaji vijana wa Arsenal baada ya winga huyo wa zamani wa Chelsea, pamoja na Gabriel waliyeanza kwa pamoja kung'ara dhidi ya Fulham.

Willian alikuwa mchezaji wa kwanza, tangu Ray Parlour mwaka 1992 kutoa pasi za mwisho mbili, kwenye mchezo wa kwanza wa ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu ya England kwa Arsenal, wakati alipowatengenezea Gabriel na Pierre-Emerick Aubameyang kwenye ushindi wa 3-0, huku Alexandre Lacazette akifunga bao jingine pale Craven Cottage.

Arteta alianza vizuri msimu mpya wa ligi hiyo, Jumamosi wakati alipomwanzisha nyota huyo mwenye umri wa miaka 32 ambaye alisaini miaka mitatu baada ya kuondoka Chelsea kama mchezaji huru, kuongeza nguvu kwenye kikosi hicho kilichojaa vijana.

Kiwango cha Jumamosi, kinamfanya Arteta aamini, kimethibitisha namna gani Willian atakavyokuwa kwa mabingwa hao wa FA.

"Willian, unaweza kuona alitaka zaidi," alisema Arteta.

"Kwa mara nyingine alionyesha kiasi gani anataka na kiasi gani atakwenda kujaribu, ili kufanikiwa.

"Ilikuwa ni kile tulichokitarajia. Tulihitaji mchanganyiko, tuna wachezaji wengi vijana wenye vipaji vikubwa na wenye majaliwa makubwa ya baadaye, lakini wanahitaji watu wa mfano na nafikiri Willian atakuwa mmoja wao anayewazunguka.

"Hazungumzi sana kwenye vyumba vya kubadilishia nguo, lakini mara zote anazungumza akiwa uwanjani na hiyo ni njia nzuri ya kufanya."

Pamoja na kufunga, mchezaji mwingine mgeni wa Arsenal, Gabriel aliyesajiliwa kutoka klabu ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Lille alionyesha kiwango cha kuvutia kuwasaidia 'Washikabunduki' hao kuondoka bila nyavu za lango zao kutikiswa na Arteta anaamini raia huyo wa Brazil hatakuwa na shida kuzoea Ligi Kuu ya England.

"Tulimfuatilia sana. Ana ubora wa aina yake na kutaka acheze na kuweza kuzoea haraka," alisema Arteta.






# Pirlo ataka straika mpya Juventus

**TURIN,** Italia

KOCHA Mkuu wa Juventus, Andrea Pirlo amebainisha umuhimu wa kusajili straika mpya, kabla ya kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Mabingwa hao watetezi wa Italia, hawana namba tisa anayetambulika kuelekea msimu mpya wa 2020-21, baada ya Gonzalo Higuain kukaribia kujiunga na Inter Miami ya Marekani.

Usajili wa nyota wa Barcelona, Luis Suarez umeripotiwa kuzuiwa, huku straika wa Chelsea, Olivier Giroud alikanusha taarifa za kuelekea kwa 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin.

Edin Dzeko, pia amekuwa akihusishwa kutua hapo, lakini alikuwa kwenye kikosi cha Roma kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Cagliari, Jumamosi ambapo walishinda.

Huku pazia la ligi hiyo likitarajiwa kufunguliwa wiki tatu zijazo, Pirlo amebainisha kwamba wanatakiwa kujaza nafasi hiyo.

# Mourinho: Bado nahitaji straika

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amezungumzia kuhusu usajili wa straika mpya, lakini amesisitiza haikuwa sababu ya kipigo cha Jumapili kutoka kwa Everton, wakati alipoulizwa kuhusu klabu hiyo kumwania Alexander Sorloth.

Spurs walipoteza kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu kwa kichapo cha bao 1-0, kutoka kwa Everton katika dimba la Tottenham Hotspur wakati, Dominic Calvert-Lewin alipofunga kwa kichwa dakika ya 55.

Hilo limekuja siku kadhaa baada ya Mourinho kuelezea umuhimu wa mshambuliaji mpya, ili kusaidiana na Harry Kane.

Sorloth ambaye anacheza kwa mkopo kule Trabzonspor anaonekana kuwa chaguo la Spurs, kwa mujibu wa Rais wa klabu hiyo ya Uturuki, Ahmet Agaoglu.

Straika huyo wa Norway alisaini mkataba wa mkopo wa miaka miwili na Trabzonspor mwaka jana, baada ya kuwa na wakati mgumu kule Crystal Palace, lakini alifunga mabao 24 katika msimu wa 2019-20 na kuwafanya Tottenham na RB Leipzig kumuwania.

Agaoglu aliiambia Fanatik: "Sorloth anataka kwenda. Lakini, hatuwezi kukubali haraka hivyo kwa kila mchezaji anayetaka kuondoka.

"Tunakutana na Leipzig na Tottenham, sisi wenyewe na Crystal Palace. Wote tunataka uhamisho huo ufanikiwe, tutafanya maamuzi kwa manufaa ya Trabzonspor."

Mourinho amesema hatazungumzia suala la usajili, lakini angependa kumchukua Sorloth.

"Sitamzungumzia Sorloth," aliwaambia waandishi wa habari. "Kama rais wa Trabzonspor amesema hivyo, nitasema si kweli.

"Nafikiri Sortloth ni mchezaji wa Trabzonspor na mimi sitakiwi kuulizwa kuhusu hilo."

Aliongeza: "Tunahitaji straika? Ndio. Kwa sababu tumepoteza mchezo? Hapana. Hatukupoteza mchezo kwa sababu tunahitaji straika."






# ALABA AONYWA DAU LA MKATABA MPYA BAYERN

**MUNICH,** Ujerumani

DAVID Alaba hatakiwi kuacha fedha itawale kichwa chake wakati huu akiwa kwenye majadiliano ya kuongeza mkataba mpya na Bayern Munich, Rais wa zamani wa klabu hiyo, Uli Hoeness ameonya.

Mlinzi huyo kisiki, Alaba anawakilishwa na wakala wake, Pini Zahavi ambaye mchezaji wa zamani, katika mazungumzo ya kusaini mkataba mpya, huku wa sasa ukitarajia kumalizika mwishoni mwa msimu wa 2020-21.

Hata hivyo, Hoeness ameonyesha kwamba majadiliano hayo hayaonyeshi kuendelea mbele na kufikia muafaka, na amesema Alaba anatakiwa kuamua kuhusu majaliwa yake wapi anataka kwenda kukaa kwa miaka mingi.

Hoeness aliiambia Sport1 Jumapili, wakati alipoulizwa kuhusu Alaba mwenye umri wa miaka 28 na akasema: "Tunamtaka abaki kwa sababu ni mchezaji wa kiwango cha juu."

"Nilikunywa naye kahawa wiki chache zilizopita, lakini bado hajafikia kwenye makubaliano ya mwisho.

"Hansi Flick anataka abaki kwenye kikosi chake."

# *Nuno ajifunga Wolves hadi 2023*

**LONDON,** England


NUNO Espirito Santo amesaini mkataba mpya na Wolves, ambao utamuweka hapo hadi mwaka 2023.

Raia huyo wa Ureno alichaguliwa kuwa kocha pale kwenye dimba la Molineux, Mei mwaka 2017 na amekuwa na wakati mzuri hapo tangu Wolves ilipopanda Ligi Kuu.

Nuno amewaongoza mara mbili mfululizo kumaliza nafasi ya saba, kwenye msimamo wa Ligi Kuu, huku pia aliishia robo fainali kwenye Kombe la Europa msimu uliopita.

"Najihisi vizuri. Tayari kwa hilo. Nikiangalia mbele. Kufanya kazi kwa bidii kwa sababu ni mzunguko mpya, bila kujua nini ulichokifanya kabla," alisema akinukuliwa na tovuti ya Wolves.

Huku akiwa na wachezaji kama Ruben Neves, Adama Traore, Joao Moutinho na Raul Jimenez pale kwenye dimba la Molineux, Nuno anaonekana kocha ambaye anaweza kupata mafanikio makubwa zaidi kwa siku sijazo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR AJUTA KUTOMTIA NGUMI YA USONI ALVARO

Ni wakati akilimwa kadi nyekundu PSG ikilala tena, asema kitu pekee anachoweza...

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR amesema kitu pekee anachokijutia ni kutompiga ngumi ya uso Alvaro, baada ya kutolewa nje kwa kadi nyekundu wakati Paris Saint-Germain ikifungwa na Marseille kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Jumapili.

Nyota huyo wa Brazil alikuwa mmoja wa wachezaji watano walioonyeshwa kadi nyekundu kwenye mchezo huo, ambao ulimalizika kwa vurugu kubwa katika dakika tisa za nyongeza pale katika dimba la Parc des Princes.

**Neymar alionekana akimshutumu mlinzi Alvaro kwa kumtamkia maneno ya ubaguzi wa rangi, wakati akizungumza na mwamuzi wa nne alipokuwa anaondoka uwanjani, na marudio ya video yalionyesha aliamua kumpiga ngumi nyuma ya kichwa.**

Baada ya mchezo huo, Neymar aliposti kwenye Twitter, akiandika kwamba alitakiwa kumpiga ngumi ya uso beki huyo wa Marseille.

"Kitu pekee ninachojutia ni kutompiga ngumi ya uso," aliandika.

Waliotokea benchi kwa PSG, Leandro Paredes na Layvin Kurzawa walionyeshwa kadi nyekundu, huku pia nyota wa Marseille, Jordan Amavi na Dario Benedetto, walikuwa miongoni mwa walioonyeshwa kadi nyekundu pamoja na Neymar.

Bao pekee la Florian Thauvin alilowafunga PSG, liliwafanya kupoteza mchezo wa pili mfululizo kwa mara ya kwanza, wakati wa ufunguzi wa ligi hiyo tangu msimu wa 1984-85.

## ZISIKUPITE

### UNITED NJIA NYEUPE KWA BALE

MANCHESTER United itapaswa kulipa kiasi cha pauni milioni 18.5 pekee, ikiwa wanataka kumsajili winga wa Real Madrid na Wales, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 31. ***(Mundo Deportivo)***

### INGS AWINDWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inawania kumsajili mshambuliaji wa Southampton, Muingereza Danny Ings mwenye umri wa miaka 28. ***(Football.London)***

### COSTA MGUU SAWA KUUZWA

MCHEZAJI Douglas Costa amewekwa tayari kuuzwa na Juventus. Manchester United awali walikuwa wakihusishwa na taarifa za kumtaka winga huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 29. ***(Goal)***

### ERIKSEN KUONDOKA INTER

KIUNGO wa kati wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 28, anaweza kuruhusiwa kuondoka Inter Milan, ikiwa ni miezi kadhaa tu tangu kujiunga na klabu hiyo akitokea Tottenham. ***(Calciomercato)***

### ARSENAL YAMWINDA RINAR

ARSENAL inataka kumsajili mlinda mlango wa Iceland, Rinar Runarsson mwenye umri wa miaka 25, na imeanza mazungumzo na klabu yake ya Dijon kuhusu mpango huo. ***(Telegraph)***

### PORTO YASHUKA KWA ALEX

KLABU ya Porto FC imepunguza bei ya beki wake wa kushoto rai wa Brazil, Alex Telles hadi pauni milioni 18.5, huku Manchester United ikimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(A Bola)***

### SPURS, UNITED KWA REGUILON

TOTTENHAM inaweza kuchuana na Manchester United kuwania saini ya mlinzi wa kushoto wa Real Madrid na Hispania, Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 23. ***(Mail)***

### KUMBULLA AGOMBEWA EPL

KLABU ya Tottenham imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kuwania kumsajili mlinzi wa Hellas Verona, Marash Kumbulla. Chelsea na Manchester United wamehusishwa na taarifa za kutaka kumnasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20. ***(L'Arena, via Sun)***

### NEWCASTLE YAMFUATA CENGIZ

KLABU ya Newcastle inataka kumchukua winga wa Roma na Uturuki, Cengiz kwa mkopo. Leicester pia inavutiwa na mchezaji huyo wa miaka 23. ***(Inside Futbol)***

### SARLOTH AWANIWA SPURS

TOTTENHAM pia wapo kwenye mazungumzo na Trabzonspor kwa ajili ya mpango wa kumpata mshambuliaji, Alexander Sorloth. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, anacheza kwa mkopo wa miaka miwili akitokea Crystal Palace. ***(Express)***

### BROOKS SOKONI B'MOUTH

KLABU ya Bournemouth imeiambia Leicester kuwa, watapaswa kulipa pauni milioni 50 kumpata kiungo wa kati, David Brooks mwenye umri wa miaka 23. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

## Baraza apania kuibana Simba

**NA Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Biashara United, Francis Baraza, amesema anaendelea kuwapa mbinu zaidi wachezaji wake kulingana na kila mchezo wanaoenda kukabiliana nao ili kuweza kuendeleza ushindi katika mechi zao za Ligi Kuu Bara msimu huu.

Biashara United ni miongoni mwa timu nne zenye alama sita kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara baada ya kushinda mechi zao mbili za raundi ya kwanza; nyingine ni KMC FC, Azam FC na Dodoma Jiji FC.

Juzi Biashara United ikiwa katika uwanja wao wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma iliichapa Mwadui FC ya Shinyanga kwa bao 1-0, sawa na ushindi walioupata kwenye mechi yao ya ufunguzi walipoikaribisha Gwambina FC ya Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu kutoka mkoani Mara jana, kocha huyo alisema katika mchezo ujao dhidi ya Simba Jumapili, atahakikisha anapata matokeo mazuri ili waweze kuendelea kukaa nafasi za juu.

Baraza alisema anaiheshimu timu hiyo kwa kufahamu ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ikiwa ni pamoja na bingwa wa Kombe la Shirikisho (FA Cup), jambo ambalo litawafanya kuingia uwanjani kwa tahadhari kubwa.

## Uwanja wa Karume nao wafungiwa

**Na Adam Fungamwango**

IKIWA imekamilika raundi ya pili tu ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21, Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB) imeifungia Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume uliopo Musoma mkoani Mara kuchezewa mechi yoyote ile ya mashindano kutokana na ubovu wa eneo la kuchezea na vyumba vya kubadilishia nguo kutokidhi vigezo.

Taarifa kutoka Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi hiyo kwenda kwa vyombo vya habari jana ilisema kuwa Bodi imetoa siku 21 kwa wahusika kufanya marekebisho ya uwanja huo kwenye maeneo yaliyoainishwa kabla ya Kamati ya Leseni haijapita kufanya ukaguzi.

Taarifa hiyo, Bodi imeitaka klabu ya Biashara United ambayo timu yake inatumia uwanja huo kama wa nyumbani, kupendekeza uwanja mwingine mbadala ulio jirani, kama vile CCM Kirumba ama Nyamagana, vyote vipo mjini Mwanza.

Taarifa hii ya Bodi ya Ligi imekuja siku mbili tu baada ya Bodi hiyo kuufungia Uwanja wa Gwambina uliopo Misungwi mkoani Mwanza, kutokana na sehemu yake ya kuchezea kutokuwa na hali nzuri, kinyume cha kanuni, na pia kuitaka klabu ya Gwambina kuchagua viwanja vya CCM Kirumba ama Nyamagana kwa ajili ya kuchezea ligi.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Bodi hiyo, Almasi Kasongo amesema kuwa viwanja hivyo vimefungiwa kutokana kutokidhi sheria namba moja ya soka inayohusiana na uwanja, lakini pia kanuni namba saba ya Ligi Kuu ambayo nayo inahusu uwanja unatakiwa uwe vipi.

# SARPONG AKIRI LIGI KUU BARA NGUMU

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya kwamba ndiyo kwanza amecheza mechi mbili za Ligi Kuu Bara, mshambuliaji hatari wa Yanga, Mghana Michael Sarpong, amekiri ligi hiyo ya Tanzania ni ngumu na yenye ushindani mkali.

**Sarpong aliifungia Yanga bao la kusawazisha wakati ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Tanzania Prisons kwenye mechi ya ufunguzi ya Ligi Kuu Bara Septemba 6, mwaka huu katika Uwanja wa Mkapa.**

Hata hivyo, licha ya kuhaha kutaka kuendeleza kasi yake ya kucheka na nyavu, juzi alishindwa kufua dafu mbele ya mabeki wa Mbeya City katika mchezo wao wa raundi ya pili uliopigwa Uwanja wa Mkapa na Yanga kushinda kwa bao 1-0 dakika za mwisho.

Bao hilo pekee la Yanga lilifungwa kwa kichwa na beki wa kati, Mghana Lamine Moro akiutendea haki mpira wa kona uliochongwa na kiungo Muangola Carlos Carlinhos dakika ya 86.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Sarpong alisema lengo lake ni kuipa mafanikio timu yake kwa kuiwezesha kushika nafasi ya juu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini ligi hiyo ni ngumu na yenye ushindani mkubwa.

"Ligi ya Tanzania ina ushindani mkubwa, kutokana na kila timu kujipanga kupata matokeo mazuri pindi inapokuwa uwanjani, ninaona jinsi timu zilivyojipanga vizuri kila moja inataka kushika nafasi ya juu," alisema Sarpong.

Kuhusu mechi hiyo ya juzi, alisema ilikuwa ngumu, lakini ameshukuru timu yake kuondoka na pointi tatu uwanjani.

Akizungumzia ushindani wa namba, Sarpong alisema ni mkubwa katika kikosi chao, lakini atazidi kujituma kwa nguvu zote kila akipata nafasi ili kujihakikishia kucheza na kuipa mafanikio timu kama alivyoahidi kipindi anatua nchini.

"Ninashukuru wachezaji wenzangu wamenionyesha ushirikiano kuanzia nilipofika sijaona tofauti yoyote, ninaahidi mashabiki wangu kufanya vizuri," alisema.

Aidha, aliwataka mashabiki na wanachama wa Yanga kuendelea kumpa sapoti ili aweze kuipa ushindi timu yake pindi watakapokutana na Kagera Sugar, Jumamosi ijayo katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

MILIKI...



Mshambuliaji na nahodha wa Simba, John Bocco, akimiliki mpira dhidi ya mabeki wa Mtibwa katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro Jumamosi iliyopita na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **MPIGAPICHA WETU**

## *Amri alia na mabeki bao la usiku Yanga*

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushuhudia kikosi chake kikikubali kipigo cha bao la usiku (dakika za mwisho) juzi, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Amri Saidi, amesema kitendo cha mabeki kushindwa kuwa makini dhidi ya beki wa Yanga, Lamine Moro na kumuacha aruke peke yake na kufunga kwa kichwa, ndicho kilichowagharimu.

Mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Mkapa juzi, ilionekana kama ingemalizika kwa sare tasa, lakini kukosa umakini kwa mabeki wa Mbeya City, kuliwagharimu katika dakika ya 86 baada ya Lamine kuruka peke yake na kuunganisha nyavuni mpira wa kona uliopigwa na kiungo Muangola Carlos Carlinhos, hivyo kuiwezesha Yanga kuibuka na ushindi wa bao 1-0.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Saidi alisema wachezaji wake walifuata maelekezo na kufanikiwa kuvunja mipango ya Yanga kwenye dakika 80 ya mchezo huo, ila kutokuwa makini kwa walinzi wake ndiko kulikosababisha kupoteza mchezo huo.

Alisema walitengeneza mipango yao na kufanikiwa hali ambayo iliwafanya wapinzani wao kusubiri hadi dakika za mwishoni kuweza kupata bao la ushindi baada ya kutumia makosa waliyofanya kuwaadhibu.

"Niliendaa kufanyia kazi mbinu zao baada ya kuwaona wakicheza na Tanzania Prisons," alisema kocha huyo.

Beki huyo wa zamani wa Simba na Taifa Stars, alisema baada ya kuona mapungufu hayo, anaenda kuyafanyia kazi na kuhakikisha kikosi cha timu yake hiyo kina kuwa imara zaidi katika michezo ijayo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Michezo
Jumanne Septemba 15, 2020
Nipashe




Neymar ajuta kutokumpiga Alvaro UKURASA 22

# ZLATKO: SIRI CARLINHOS KUPIKA BAO YANGA SC

## ●●● Afunguka alichomtuma kuifanya Mbeya City, atoa sababu pia timu hiyo kupoteana...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kumpa nafasi kwa mara ya kwanza katika mechi ya Ligi Kuu Bara tena kwa dakika 29 tu kabla ya mechi kumalizika, lakini akaonyesha umuhimu wake uwanjani dhidi ya Mbeya City juzi, Kocha Mkuu wa Yanga, Zlatko Krmpotic ametoa siri ya kiungo wake, Muangola Carlos Carlinhos kuibeba timu na kuibuka na ushindi kwenye mechi hiyo.

**Carlinhos aliingia akitokea benchi dakika ya 61 kuchukua nafasi ya Feisal Salum 'Fei-Toto', ambapo mbali na mashuti yake mawili kushindwa kujaa nyavuni, kona yake ya dakika ya 86 kutoka wingi wa kushoto, iliunganishwa kimyani kwa kichwa na beki wa kati, Mghana Lamine Moro, bao lililoiwezesha Yanga kushinda 1-0 katika Uwanja wa Mkapa juzi.**

Akimzungumzia kiungo huyo pamoja na maelekezo aliyompa katika mchezo huo, Zlatko alisema Carlinhos ana uwezo mkubwa na pia aliingia uwanjani na kufuta makosa ya mtu aliyechukua nafasi yake kwa kutendea haki mipira ya kona, faulo pamoja na kupiga mipira mirefu.

"Nilimpa maelekezo ya kuhakikisha anafanya majukumu yake vema kwa kuhakikisha mipira ya kona na faulo inakuwa na faidi kwetu, jambo ambalo alifanikiwa na kusababisha bao lililofungwa na Lamine Moro," alisema kocha huyo raia wa Serbia aliyechukua nafasi ya Mbelgiji Luc Eymael, ambaye alitimuliwa mwishoni mwa msimu uliomalizika.

Kuhusu mchezo mzima ulivyokuwa, Zlatko kwanza aliwasifu wachezaji wake kwa kupambana kupata matokeo hayo, lakini akaeleza bado anahitaji kupata muda na timu hiyo ili kuiwezeha kucheza kwa muunganiko mzuri.

Zlatko alisema mechi ilikuwa ngumu sana kwa sababu wapinzani wao walikuja kutafuta sare, lakini kwa upande wao walihitaji kupata matokeo chanya ambayo wachezaji walipambana kufanikisha.

Alisema kipindi cha kwanza wachezaji wake hawakucheza vizuri kama alivyotarajia jambo ambalo alilazimika kufanya mabadiliko kidogo katika dakika 20 za mwisho kwa kuwataka kucheza kwa kushambuliaji zaidi.

"Mechi ilikuwa ngumu sana, wachezaji wangu walipambana kupata matokeo, ila bado hawajacheza vizuri kama nilivyotarajia na timu haina muunganiko mzuri, hii inatokana na kutopata muda wa kujiandaa kwa msimu mpya," alisema Zlakto.


Alisema ana imani atatumia mechi hizo za ligi kutafuta ushindi, lakini kukiweka imara kikosi chake.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM, wanaoidhamini Yanga, Mhandisi Hersi Said, mbali na kumsifu Carlinhos, alisema ushindi huo ni mwelekeo mzuri wa kufanya vizuri katika michezo yao ijayo kwa sababu malengo yao msimu huu ni kupata matokeo chanya kila mechi.

"Leo kocha amempa dakika 30 Cralinhos, tuna imani mechi ijayo atamwongezea dakika na ataonyesha kitu kizuri, tumeshinda ila tunaona bado timu yetu haijapata muunganiko mzuri na kila tunapozidi kucheza mechi timu inaimarika," alisema Hersi.

Yanga itashuka tena dimbani Jumamosi wiki hii, lakini wakati huu ikiwa ugenini katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoka kuvaana na wenyeji wao, Kagera Sugar ambayo imetoka kulazimishwa sare tasa ugenini dhidi ya Gwambina FC ikiwa ni baada ya mechi ya ufunguzi kuchapwa 1-0 nyumbani na JKT Tanzania.

**TULIA WEWE!...**




Mshambuliaji wa Yanga, Mghana Michael Sarpong, aking'ang'aniwa na mchezaji wa Mbeya City, wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Mkapa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Morrison kuiingizia TFF mil.15/-

**Na Adam Fungamwango**

SAKATA la kesi ya kiungo Mghana Bernard Morrison linaweza kuliingizia Shirikisho la Soka nchini (TFF), kiasi cha Sh. milioni 15, baada ya Kamati yake ya Maadili, kuwatoza faini hiyo wasemaji wa Klabu ya Simba na Yanga, Haji Manara na Hassan Bumbuli pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Simba, Zacharia HansPope, imeelezwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili ya TFF, Wakili Kichere Mwita Waissaka, jana jijini Dar es Salaam wakati akitangaza uamuzi uliofikiwa baada ya kamati hiyo kuketi, aliwaambia waandishi wa habari kuwa watajwa hao watatu, kila mmoja atalipa Sh. milioni tano, lakini wanatakiwa kutotenda kosa lolote la kimaadili ndani ya miaka miwili.

Manara ambaye ni Ofisa Habari wa Simba, amekutwa na hatia kwa kuingilia majukumu ya Kamati ya Katiba, Sheria na Hadhi za Wachezaji wakati wa kesi ya Morrison na Yanga kwa maneno aliyodaiwa kuyasema kupitia chombo kimoja cha habari, huku Bumbuli, yeye akikutwa na hatia ya kusema uongo kwa kamati hiyo wakati wa kesi hiyo, kuwa hawajapeleka nakala ya hukumu ya kamati wakati ilishafikishwa klabuni siku moja kabla ya yeye kuongea hivyo.

HansPope, amekutwa na hatia ya makosa mawili. Kwanza ni kutoa taarifa ya mwenendo wa kesi iliyokuwa ikijadiliwa huku yeye akiwa ni mjumbe wa kamati hiyo, na pili kuchochea umma kuhusu sakata la mchezaji huyo.

Hata hivyo, Wakili Kichere alisema rufani iko wazi kwa yeyote ambaye hajaridhika na hukumu ya shauri hilo.

Akizungumzia hukumu hiyo, Manara alisema: "Nikiipata nitaisoma na nitakaa na viongozi wangu wa klabu na wanasheria kuangalia kama ipo haja ya kukata rufani kwa sababu nafasi hiyo ipo, ama kama kuacha tu, hii ni baada ya kukaa na wataalamu ili nipate ushauri kutokana na adhabu hii kubwa."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >